**20 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Hamsini – Tarehe 20 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nicholaus Ngassa karibu uulize swali lako.

Na. 636

**Barabara inayounganisha Mbutu na Igunga Mjini**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kuunganisha kipande cha Mbutu na Igunga Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kipande cha barabara ya Mbutu hadi Igunga Mjini chenye urefu wa kilometa tano na imepanga kufanya usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2025/2026. Hatua hii inalenga kubaini gharama halisi za ujenzi, mahitaji ya kiufundi na kuandaa nyaraka za zabuni zitakazotumika wakati wa utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa usanifu huo, Serikali imepanga kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2026/2027 kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Kuweka rekodi sawa, kipande cha barabara ya Mbutu kwenda Igunga Mjini upande wa kushoto na kulia una lami. Ninashukuru majibu ya Serikali kwa kuwa wameamua kuchukua hatua na kuanza utekelezaji wa hii barabara, basi mimi sitakuwa na swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashauri kwamba wakikamilisha utekelezaji, watakuwa wameokoa maisha ya watu wengi kwa sababu pale kuna taasisi mbili; shule za sekondari, Shule ya Msingi ya *St. Leo* na Shule ya Sekondari ya Igunga ambapo kuna wanafunzi wengi na wanapata changamoto ya vumbi sana kipindi cha kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninashukuru majibu ya Serikali kwa kuanza huo utekelezaji, na sisi Wanaigunga tunalipokea kwa mikono miwili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nollo; kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 637

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mpalanga – Bahi**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mpalanga – Bahi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mpalanga ina vijiji vitatu ambavyo ni Mpalanga, Nholi na Chidilo na ina jumla ya watu 13,664 kwa Sensa ya Watu na Makazi ya m

waka 2022. Aidha, vijiji viwili vya Mpalanga na Chidilo vina zahati na Kijiji cha Nholi ujenzi wa zahanati unaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilipeleka shilingi milioni 60 kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa huduma za rufaa na upasuaji wa dharura zinazotokea katika Zahanati za Kata ya Mpalanga zinahudumiwa na Kituo cha Afya Chipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za kimkakati zitakazokidhi vigezo kote nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Katika Kata za Bahi, ujenzi kama ulivyosema unaendelea kufanyika kwenye vituo vya afya, lakini kuna wataalam wachache wa afya. Je, ni lini wataalam wa afya watapelekwa kwenye Kata hizo za Bahi ambapo sana ni manesi na madaktari?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kuna vituo vya afya vikongwe katika Manispaa ya Morogoro ambavyo ni Sabasaba pamoja na Mafiga. Ni lini vitapata kujengewa chumba cha upasuaji ili kupunguza tatizo linalotokea kwenye Hospitali ya Mkoa pamoja na kuwapatia akinamama huduma ambao wanapata matatizo ya kujifungua kawaida? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana kuendelea kuimarisha sekta hii muhimu kabisa ya afya msingi. Mheshimiwa Mbunge amehoji kuhusiana na uhitaji wa watumishi wa afya katika hii Wilaya ya Bahi kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inafanya jitihada ya kuajiri watumishi wa kada ya afya na kuwapanga katika maeneo tofuti tofauti katika vituo hivi vya kutolea huduma ya afya msingi ili waweze kutoa huduma hiyo bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea na jitihada hizo za kuajiri. Tayari vibali vya ajira ya watumishi hawa vinatoka kila mwaka wa fedha na watumishi hawa watapangwa katika vituo hivi alivyovitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, ninaomba nimtaarifu kwamba, Serikali inaendelea pia kuboresha miundombinu kwa maana ya ujenzi wa hospitali, kukarabati hospitali kongwe, kujenga vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya vituo vya afya 367 vimejengwa kwenye Serikali hii ya Awamu ya Sita, zaidi ya zahanati 980 zimejengwa, na hospitali za Halmashauri 129. Kwa hiyo, unaona kabisa dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendelea kuimarisha miundombinu katika vituo vyetu hivi vya kutolea

huduma ya afya msingi katika vituo hivi alivyovitaja katika Eneo la Sabasaba na hili lingine alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, Serikali itahakikisha inafika kwa ajili ya kujenga chumba cha upasuaji ili kiweze kuwanufaisha wananchi, waweze kupata huduma bora zaidi na hasa hizi za upasuaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi kwenye Kata ya Kiberashi ina vijiji saba, lakini ni vijiji vitatu vyenye zahanati, hawana kituo cha afya. Je, ni lini mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapata kituo cha afya au kwa maana hospitali kubwa ambayo inaweza kuhudumia eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahakikisha kwamba kila Halmashauri inajengewa Hospitali ya Halmashauri. Mpaka wakati huu, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Hospitali za Halmashauri 129 tayari zimeshajengwa, na Serikali inaendelea kuhakikisha kila Halmashauri inapata hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kata za kimkakati. Fedha zinapelekwa kwa ajili ya kujenga vituo hivi vya afya. Hata katika huu mwaka wa Bajeti, tulipitisha hapa Bungeni nyongeza ya bajeti shilingi bilioni 53 kwa ajili ya kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kila jimbo katika majimbo 214.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, hata kwenye Jimbo lake italetwa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuhakikisha kinajengwa kituo cha afya cha kimkakati. Serikali inaendelea pia na jitihada za ujenzi wa zahanati katika maeneo yote ambayo yana uhitaji na yanakidhi sifa ya kujengewa zahanati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Serikali ya Awamu ya Sita pekee, tayari zaidi ya zahanati 980 zimejengwa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hata Kilindi tutaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zahanati zinajengwa, vituo vya afya vinajengwa na huduma za afya msingi zinaimarishwa kwa ajili ya wananchi wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Nusrat Hanje, kwa niaba.

Na. 638

**Mabadiliko ya Tabianchi Nchini**

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED K.n.y. MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, Serikali ina Mikakati gani ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashirikiana kikamilifu na Jumuiya za Kimataifa katika kubuni mikakati na hatua madhubuti za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika ngazi zote. Baadhi ya Mikakati inayochukuliwa na nchi katika kukabiliana na athari hizo ni pamoja na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Itifaki ya Kyoto ya makubaliano ya Paris, kuandaa na kutekeleza nyenzo za kisera zitakazosaidia kutoa dira na kuibua programu na kutekeleza miradi inayosaidia jamii katika maeneo mbalimbali ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi, hii inajumuisha mikakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021), Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-

2032) na Mchango wa Taifa katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini. Miradi hii inajumuisha upandaji wa miti, usambazaji wa majisafi kwa matumizi ya majumbani na mifugo, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, matumizi ya nishati mbadala ikiwemo nishati safi ya kupikia ili kupunguza kasi ya ukataji wa misitu, ujenzi wa kuta katika maeneo ya fukwe za bahari yanayokabiliwa na mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa matuta na mabwawa kudhibiti mafuriko, kuwezesha jamii kubuni miradi mbadala ya kuongeza kipato na iliyo rafiki kwa mazingira na kurejesha maeneo ya ardhi yaliyoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na jitihada za Serikali za kuhamasisha masuala mazima ya upandaji miti mashuleni ambao wana kampeni ambayo inasema, "Soma na Mti," lakini kumekuwa na changamoto kubwa ya wananchi nje ya mashule, bado kupata taaluma hii ya suala la upandaji wa miti. Miti imekuwa inakatwa sana kiholela na kusababisha masuala mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuja na kampeni maalum kwa jamii na kuhamasisha suala zima la upandaji wa miti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kumekuwepo na uchafuzi mkubwa wa masuala ya fukwe zetu. Kuna baadhi ya hoteli wawekezaji ndani ya nchi yetu na wanaokuja, wanajenga chini ya kingo za mito, na wengine wanapewa vibali hadi kuchimba bahari. Hii inasababisha pia mabadiliko ya tabianchi, maji kuzidi kwenye kima ya bahari na kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni nini mkakati wa Serikali juu ya kutoa elimu ama kwenda nao hawa wawekezaji kuja na mpango maalumu wa kuhakikisha fukwe zetu na kingo zinahifadhiwa kwa utulivu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumefanya kasi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuelimisha wananchi juu ya suala zima la upandaji na ushughulikiaji wa miti. Moja ya miongoni mwa hatua hiyo ilikuwa ni kuanzisha Kampeni Maalum ya 'Kusoma na Mti' ambapo tuliwataka wanafunzi wote wa shule za msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu kuhakikisha kwamba wanapanda miti ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tumeendelea kutoa elimu shuleni, kwenye semina tofauti na hata kwenye makongamano yetu yanayohusiana na masuala ya mazingira, tumekuwa tukielimisha watu suala zima la kupanda miti. Kikubwa zaidi tunaendelea kutoa elimu kwenye matukio makubwa ya Kitaifa, hata matukio ya kila siku ambayo tunayafanya katika jamii kusudi tuongeze *speed* ya upandaji miti na kuokoa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na changamoto ya kuchimbwa bahari na kutokuhifadhi fukwe, ni kweli zipo shughuli zinafanyika karibu na maeneo haya ya ufukwe zikiwemo za ujenzi wa hoteli, ukataji wa miti hasa mikoko na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwaelimisha wananchi, ni kwamba tunawaomba sana wananchi Tanzania nzima waendelee kutunza fukwe na maeneo ya Bahari, lakini kubwa wazingatie ule mwongozo wetu wa mita 60, kwamba shughuli zote zinazofanyika karibu na vyanzo vya maji ikiwemo bahari, mito, maziwa na vyanzo vingine zihakikishe kwamba zinazingatia mwongozo wa mita 60. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Benardeta Mushashu.

Na. 639

**Manufaa ya Biashara ya Carbon Nchini**

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, biashara ya kununua na kuuza *carbon* imeinufaishaje Tanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni nchini ambapo jumla ya miradi 73 ya biashara ya kaboni imeshasajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo ni ya sekta za misitu 51%, nishati 33%, taka asilimia tatu, kilimo asilimia nane na mifugo asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hii huchangia katika uhifadhi na urejeshaji wa misitu na ardhi ili kuongeza fursa za ajira na pato la wananchi kwa ujumla na kupunguza uzalishaji wa gesijoto ambapo huchangia katika kufikia malengo ya utekelezaji wa mchango wa Taifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi *(Nationally Determined Contribution)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa ya kiuchumi katika baadhi ya maeneo nchini ambapo kiasi cha shilingi bilioni 45 zimelipwa na kunufaisha wananchi katika Halmashauri 10 nchini kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni. Fedha hizi hutumika katika kutekeleza miradi ya kijamii katika vijiji husika kama vile ujenzi wa shule, zahanati, malipo ya bima za afya, ada za shule na chakula kwa wanafunzi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Ili uweze kufanya hii biashara ya kuuza na kununua kaboni, ni vigezo gani vinavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Mkoa wa Kagera una mvua nyingi, na kwa sababu ya mvua hizo tuna miti na misitu mingi, kwa sababu inaonekana hii biashara ya kuuza na kununua kaboni ni biashara nzuri, ina manufaa makubwa kwa Taifa, lakini inaweza ikamnufaisha hata yule anayefanya hii biashara. Je, ni lini sasa Serikali itaenda mkoani Kagera kuhamasisha ili kusudi hawa watu nao waanze hii biashara waweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mushashu kwa kuwa amekuwa mdau mzuri wa mazingira hasa kwenye masuala haya ya kaboni. Ili tuweze kukusajili, ama uweze kusajiliwa na kuweza kufanya shughuli hizi za biashara ya kaboni, vipo vigezo ambavyo hivyo lazima vifikiwe ndipo tuweze kumpatia mtu fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tuhakikishe kwamba amepata eneo ambalo litakuwa linaweza likafanyiwa hiyo biashara. Pia, tuhakikishe kwamba awe na kampuni ambayo imesajiliwa, awasilishe andiko maalum kwenye kituo chetu cha kaboni pale Morogoro, andiko ambalo litatushawishi ama litashawishi taasisi inayosimamia kaboni kuweza kumpatia fursa kuweza kufanya hiyo biashara na ahakikishe kwamba amelipa *fee* ya usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi ahakikishe kwamba awe mzalendo wa kuhakikisha yupo tayari kufanya shughuli hizi bila ya kuathiri mazingira mengine ambayo yamezunguka wanakijiji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mkoa huo aliouzungumza, tayari elimu imeshaanza, tumeshafika huko. Kikubwa, tunaendelea kufanya bidii ya kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa wananchi sambamba na kuwaeleza faida, fursa na changamoto mbalimbali ambazo zinapatikana katika biashara hii. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Kasaka, kwa niaba yake Mheshimiwa Festo.

Na. 640

**Uhitaji wa Umeme Maeneo ya Wachimbaji Wadogo Chunya**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya juhudi za makusudi kupeleka umeme kwenye maeneo ya Wachimbaji Wadogo Wilayani Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika migodi midogo nchini ambapo katika Wilaya ya Chunya, Serikali imepeleka umeme katika maeneo ya migodi ya wachimbaji wadogo 16 kati ya migodi 18 iliyopo Wilayani hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo mawili ya migodi yaliyobaki, Mkandarasi aitwaye *OK Electrical and Electronics* anaendelea na kazi, na anatarajia kukamilisha kupeleka umeme hivi karibuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kufikisha umeme kwenye haya maeneo 16 kati ya maeneo 18. Kwa niaba ya Mbunge wa Chunya (Mheshimiwa Njelu Kasaka), anaipongeza Serikali, pia na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alikuwa kule kwa ajili ya kufungua Kiwanda cha Kuchenjua shaba ambacho kwa kweli kinategemea sana umeme. Pia tuna maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kumekuwa na changamoto ya umeme Chunya kwamba una nguvu ndogo kutokana na matumizi makubwa ya ile *line*. Ni lini Serikali itajenga *sub-station* kwa ajili ya kuongezea nguvu ili umeme huu uweze kuwafikia Wanachunya na wenye migodi hii ili wapate umeme wa uhakika wakati wa shughuli zao za uchimbaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Ni kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Makete ambalo mimi ni Mbunge wao. Ninaomba kuuliza kwamba, sisi watu wa Makete tulikuwa na changamoto ya umeme kutokea Mbeya kwenda Makete na sasa Serikali imetubadilishia kutoka Makete kwenda Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo tunaipata, umeme ni wa uhakika, lakini kumekuwa na kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara. Tunahitaji kitu kimoja kinaitwa *Automatic Power Regulator* ambapo huwa vinafungwa na Wizara. Ni lini vifaa hivyo vitafungwa ili umeme Makete usikatike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Chunya ni eneo ambalo lina utajiri mkubwa wa madini, na kutokana na hili ndiyo maana tumeelekeza nguvu ya kupeleka mradi wa gridi imara kule, lakini kasi ya kugundua madini ni kubwa sana. Hivi tunavyozungumza, tayari kuna maeneo mapya 29 wananchi

wamegundua dhahabu. Kwa hiyo, kama Serikali, tumeona umuhimu wa kuongeza nguvu katika eneo lile. Kwa hiyo, kupitia gridi imara, tunaenda kujenga *sub-station* nyingine kubwa kwa ajili ya kuongeza uwezo kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ambapo anasema kwamba kwa Makete umeme una-*fluctuate,* na kwamba kuna kifaa ambacho kinahitajika kuwekwa. Ninaomba nimhakikishie, baada ya hapa tukutane, tuzungumze, ili tuone mahitaji halisi ni yapi, halafu tuweze kuelekeza wataalamu wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hilo hilo la umeme ku-*fluctuate* linatokea katika eneo la Mipango na Miyuji kule. Je, kuna mpango gani wa kurekebisha kwa maana ni katikati ya Jiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili liko kwenye maeneo mengi nchini. Kama mnavyokumbuka, Serikali iliwasilisha taarifa hapa kwamba, moja ya changamoto kubwa ni mifumo yetu ya kusambaza umeme ambayo imechakaa na kwamba tumekuja na utaratibu huu wa kuwa na mradi wa gridi imara ili kuondoa mifumo ya zamani na kuleta mifumo mipya. Kazi hii itachukua muda kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na Subira, kwani tukiweza kukamilisha jambo hili, basi tatizo hili la *fluctuation* litakuwa limeondoka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Lucy, kwa niaba yake, Mheshimiwa Kajege. Mpira wa Simba unachezwa Simba na mpira wa Yanga unachezwa Yanga.

Na. 641

**Sera Rafiki ya Umeme kwa Vijana Wenye Viwanda Vidogo Vidogo**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE K.n.y. MHE. LUCY J. SABU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na Sera rafiki ya nishati ya umeme kwa Vijana wanaojihusisha na Uzalishaji kwenye Viwanda vidogo vidogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015, imelenga kuwezesha upatikanaji wa Nishati ya Umeme nchini kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi pamoja na kijamii kwa watu wote wakiwemo vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza sera hii, Serikali kupitia *REA,* imekamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara na sasa kazi ya kusambaza umeme katika vitongoji inaendelea. Aidha, *REA* inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi wakiwemo vijana kuhusu matumizi ya umeme kwenye uzalishaji mali hususan viwanda vidogo vidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina swali dogo. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Jimboni Mwibara, aliahidi kuwa Serikali itaweka umeme wa *solar* katika Kisiwa cha Nafuba. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka

nimhakikishie Mheshimiwa Kajege kwamba ahadi zote za viongozi wetu wakuu ni maelekezo, na Serikali itahakikisha inatekeleza ahadi ile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Gharama za uendeshaji na hasa viwandani imekuwa ni kubwa sana na zaidi ikichangiwa na gharama kubwa ya umeme. Sasa ili kuweza kuhakikisha kwamba tuna viwanda vingi nchini hasa hivi vidogo vidogo ambavyo vimeelekezwa kwenye swali la msingi, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kupitia upya gharama hizi za umeme viwandani ili kuwawezesha Watanzania wengi kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inadhibiti upandaji wa gharama za uzalishaji ni kuwa na utaratibu wa kufanya *review* ya viwango vyetu hivi mara kwa mara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Matiko, jambo analolizungumza ni jambo ambalo ndani ya Serikali sasa hivi linafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Bilakwate, kwa niaba Mheshimiwa Mwakibete.

Na. 642

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kyerwa, Nyakatuntu na Kamuli**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE K.n.y. MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga mradi wa maji wa Kyerwa, Nyakatuntu na Kamuli – Kyerwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa kimkakati katika Wilaya ya Kyerwa Mkoa wa Kagera. Kazi zinazotarajiwa kufanyika kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji katika Mto Kagera, ujenzi wa matanki yenye jumla ya ujazo wa lita 3,300,000, ulazaji wa bomba mbalimbali zenye urefu wa kilometa 225, sanjari na ujenzi wa vituo 75 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi 18 ambapo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 168,670 waishio kwenye vijiji 37 vilivyopo kwenye Kata Saba za Kyerwa, Nyakatuntu, Nyaruzumbura, Kitwe, Businde, Bugala, na Kamuli, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, ninauliza maswali mawili ya nyongeza. Mradi huu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kyerwa ameuzungumza kwa zaidi ya miaka miwili hapa Bungeni, mimi nikiwa shahidi, na sasa Serikali inasema inakwenda kutekeleza kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba *commitment* ya Serikali, kwamba ni kweli utekelezwa mwaka ujao wa fedha, ukizingatia kwamba miaka miwili yote majibu ya Serikali ilikuwa ni kwamba imepangwa kwenye bajeti na huwa haitekelezeki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wananchi wa Jimbo la Busokelo tumekuwa na miradi zaidi ya mitano inayotekelezeka ndani ya lile Jimbo, lakini kwa muda mrefu haijakamilika. Ni lini Serikali inakwenda kukamilisha miradi hii hususan katika Kata za Luteba, Segese, Kandete, Mpombo, pamoja na Lwangwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mwakibete, nimwambie kwamba, katika bajeti ya mwaka 2025/2026 ambayo imepitishwa juzi, Waheshimiwa Wabunge wameiridhia, na jumla ya shilingi trilioni 1.06 ziliidhinishwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba, miradi yote ambayo ilikuwa labda inasuasua kwa namna moja ama nyingine, inakwenda kukamilishwa kwa wakati ili iweze kunufaisha, kwa maana kwamba wananchi waweze kunufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, na hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali, kwamba miradi yote fedha hizi ambazo Wabunge wameziidhinisha ndizo zitakwenda kukamilisha miradi yote ambayo ipo katika Jimbo hilo la Busokelo na maeneo mengine yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Thea.

Na. 643

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Mji wa Geita**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji katika Mji wa Geita uliosainiwa Mwaka 2022 utakamilika na kuanza kutoa huduma ikizingatiwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 katika Mji wa Geita unaohusisha ujenzi wa dakio katika Ziwa Victoria, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 109 pamoja na ujenzi wa matanki matano yenye jumla ya ujazo wa lita 8,900,000. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 54% ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025 na kunufaisha zaidi ya wananchi 361,000 wa Mji wa Geita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza. Mradi wa maji katika Kata ya Maposeni ni muda mrefu sasa tangu maagizo yalipotolewa, tena na Waziri Mkuu. Ni lini sasa Kata ya Maposeni itapata maji?

**NAIBU SPIKA:** Hiyo Kata iko hapahapa kwa Kanyasu au yako wewe? Mheshimiwa Dkt. Thea kama yako sema ni wilaya gani kwa maana huyu Naibu Waziri hawezi kujua yote hayo. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Maposeni ipo Jimbo la Peramiho, Songea Vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mwanza sasa tupo Songea. Mwambie bajeti imeshapita, mradi unakwenda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti imeshapitishwa na Wabunge hawa na tutakwenda kutekeleza kuhakikisha kwamba tunamaliza mradi huo, ahsante. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hayo ndiyo majibu ya Serikali, majibu *firm*. *(Kicheko)*

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Juliana Shonza, kwa niaba yake Mheshimiwa Sekiboko.

Na. 644

**Mradi wa Maji wa Mto Momba**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, lini kazi ya kuleta maji ya Mto Momba katika Miji ya Tunduma, Mlowo na Vwawa itaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa Mradi wa Maji Tunduma kwa kutumia maji ya Mto Momba kwa gharama ya shilingi bilioni 119.95 ambao utanufaisha pia Miji ya Vwawa, Mlowo sanjari na vijiji 31 vya Wilaya ya Momba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji katika Mto Momba chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 21.5, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji *(treatment plant)* wenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 20, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 317, sanjari na ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mradi huo upo kwenye hatua za awali za utekelezaji ambapo muda wake wa utekelezaji ni miezi 18 na kukamilika kwake utanufaisha wananchi 1,245,406 wa maeneo hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri na ninampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha ule

mradi wa miji 28 kutoka Same mpaka Korogwe. Watu wa Tanga tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, shida ya maji katika Wilaya za Lushoto, Korogwe Vijijini na Kilindi, bado tatizo lipo. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watu wa Kilindi, Lushoto, na Korogwe, wanaendelea kufurahia matunda ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, azma, malengo na makusudio ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba inapeleka huduma za jamii kwa wananchi wote Tanzania, mijini na vijijini ili wananchi waondokane na shida hii ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo yote ya Lushoto, Kilindi na maeneo mengine, yapo katika ilani, na fedha zimeshaidhinishwa, na maji yatafika huko. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atapeleka maji huko, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Hasunga. Mheshimiwa Hasunga, ninaona umesimama.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majibu ya Serikali yanasema kwamba mradi huu utakamilika kwa muda wa miezi 18, je, katika kipindi hicho, maji hayo yatafika kwenye eneo la Vwawa na Mlowo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kwamba, maji haya yatakapokamilika ama mradi huu utakapokamilika, Serikali kupitia Wizara ya Maji tutahakikisha kwamba maji haya yanafika

kila ambapo wananchi wapo, ama kila ambapo wahitaji wapo, ili maji haya yaweze kuwafikia wananchi. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, kila patakapokuwa pana uhitaji wa maji haya kwa wananchi, maji yatafika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Na. 645

**Kusambaza Maji ya *DAWASA* katika Mitaa ya Jimbo la Mbagala**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, lini maji ya *DAWASA* yatasambazwa Jimbo la Mbagala Mitaa ya Majimatitu, Machinjioni, Serenge, Changanyikeni, Vikunai, Kongowe na Masaki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitaa ya Jimbo la Mbagala inapata huduma ya majisafi na salama isiyo toshelevu kupitia mtambo wa mtoni, sanjari na visima virefu 29 vya maji vilivyopo Mianzini, Nzasa I, Nzasa II, Machinjioni, Kongowe I, Kongowe II, Goroka I, Goroka II na Serenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika jimbo hilo, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026, itafanya usanifu wa mradi wa kutoa maji kutoka Kisarawe II kwa lengo la kunufaisha mitaa ya Kongowe, Vikunai na Changanyikeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kutumia maji ya Mto Rufiji kwa ajili ya kunufaisha mikoa

ya Pwani, Lindi, na Dar es Salaam. Mradi huo upo kwenye hatua ya usanifu ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2025 na kunufaisha mikoa tajwa ikiwemo Jimbo la Mbagala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Je, ni lini mradi wa maji wa Kata za Imbaseni, Maji ya Chai, Kikatiti mpaka Maroroni kule Arumeru Mashariki utamalizika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshaeleza katika majibu mengi ya msingi ambayo tumeyajibu hapa kwamba bahati nzuri sana bajeti yetu imeshakamilika na Waheshimiwa Wabunge mmepitisha hapa fedha kupitia Wizara hii ya Maji takribani shilingi trilioni 1.06 mmeziidhinisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Watanzania wote, kupitia fedha zile zitakwenda kukamilisha miradi, zitakwenda kufikisha maji, zitakwenda kuondoa changamoto yote ya upatikanaji wa majisafi na salama katika nchi yetu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mifugo. Mheshimiwa Saputu.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Noah Lemburis.

**NAIBU SPIKA:** Sijakuita lakini. Haya Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Na. 646

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Maziwa Likiushin Mnadani-Arumeru Magharibi**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO K.n.y. MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Maziwa Kijiji cha Likiushin Mnadani - Arumeru Magharibi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa maziwa kwa kuweka miundombinu muhimu ya ukusanyaji ili kurahisisha upatikanaji wa maziwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha hilo, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2022/2023 ilitenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga vituo 10 vya kukusanyia maziwa ikiwa ni pamoja na Kituo cha Maziwa cha Likiushin, Arumeru Magharibi ambapo kwa sasa ujenzi wa kituo hicho umekamilika kwa 100% na Mkandarasi ameshakabidhi kituo hicho kwa Serikali kwa ajili ya kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kukamilisha miundombinu ya utunzaji wa maziwa taratibu za ununuzi na usimikaji wa tenki la kupozea maziwa na *generator* zinaendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa kweli nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo inaendelea kuboresha maisha ya Watanzania. Nina maswali mawili. Je, ni lini Kiwanda kitatengenezwa hapo ili kazi ya uchakataji na kuongeza thamani ya maziwa itekelezwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kule Meru wananchi wameanzisha taasisi yao inaitwa UWAWAME (Umoja wa Wakulima na Wafugaji Meru) kwa lengo la kuunganisha nguvu ili wajenge viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuunga mkono juhudi za wananchi hawa ili wafanikishe ndoto yao kulingana na azma ya Serikali pia ya kutaka kufanya kilimo cha biashara na ufugaji wa biashara? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru, naendelea kupokea pongezi kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa inayofanyika. Naendelea kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu kiwanda au viwanda vya kuchakata maziwa. Ni kwamba, Serikali imezidi kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao ya mifugo na mazao mengine ya shambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali, tukizingatia hii dira ambayo ni mpya tunayokwenda kuizindua ya mwaka 2050, tumehakikisha tumeweka mazingira mazuri kwa maana ya kupeleka miundombinu ya maji, umeme na barabara kwenye maeneo mbalimbali nchini, ili kuvutia wawekezaji waweze kuwekeza kila eneo kutokana na mazao wanayozalisha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mazao ya kutoka shamba na mazao ya mifugo, ikiwemo uchakataji wa maziwa, ni moja ya

mkakati madhubuti ambao Serikali imekwenda kuuweka. Tunakwenda kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika bidhaa zinazozalishwa na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, Serikali imezidi kutoa mikopo kwa wafanyabiashara, *especially,* akinamama, walemavu, vijana na watu wengine wote ili kwenda kuwekeza. Ili waweze kupata mikopo ya 10% inayotokana na halmashauri tunawashauri, hawa wakulima waungane kuomba ili waweze kuwekeza kwa ajili ya kuchakata maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile juzi Mheshimiwa Rais alipokuwa Mkoani Simiyu, amezindua chanjo ya mifugo pamoja na kutoa ruzuku kwenye mifugo kwa ajili ya kuwafanya wawekezaji au wanaowekeza kwenye mifugo waweze kupata mikopo mbalimbali ili kupata tija katika kuwekeza katika masuala yote ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kaboyoka.

Na. 647

**Ujenzi wa Barabara ya Mroyo – Ndungu – Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, lini lami itawekwa kwenye Barabara ya kutoka Mroyo hadi Ndungu, Wilayani Same.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Mroyo – Ndungu kilomita 5.2 inaendelea na

utekelezaji wake, kwa sasa umefikia 72%. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika tarehe 27 Novemba, 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, kupande hiki cha Mroyo – Ndungu kimetandazwa kokoto ambazo magari mengine yakipita, haya yaliyopo nyuma yanavuviwa vioo, kwa ajili ya zile kokoto zinarukaruka sana, na Kwa kuwa, pembezoni mwa hii barabara kwa mwaka wa nne huu kumewekwa udongo ambao naamini ulikuwa ni mchanga na umeota majani, je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua za dharura kusaidia kuondoa huu udongo kwa sababu hata gari lililopo nyuma ambapo kokoto zinarukaruka, haliwezi hata kukwepa zile kokoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Serikali imeshatoa malipo ya awali kwa kipande hiki cha Ndungu – Mkomazi kwa mkandarasi, na kwa kuwa, mkandarasi huyu ameshaweka kambi ile, je, Serikali inamsimamia mkandarasi kwamba, aanze hiyo kazi ya kuweka lami wakati gani au kipindi kipi kinachokuja? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Kaboyoka kwa jinsi ambavyo anasimamia eneo lake na kuhakikisha kwamba, tunatekeleza vizuri majukumu yetu. Natumia nafasi hii pia kumkumbusha Mheshimiwa Kaboyoka kwamba, awali wananchi wa Kilimanjaro, hususan Same, walikuwa wanaiomba Serikali ikamilishe au ianze ujenzi wa mradi huu, lakini huko nyuma hatukuweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua rasmi kuijenga barabara hiyo kwa maslahi ya Taifa letu, lakini kwa sasa hivi mkandarasi hajalipwa, hivyo kazi imesimama

kidogo kwa kuwa ni muhimu pale tunapokuwa na miradi, barabara hizo zipitike bila kuleta usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu au Mtendaji wa *TANROADS,* kupitia Meneja wa Mkoa husika wa Kilimanjaro, aende katika eneo husika atazame changamoto inayozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge. Kama kutakuwa na changamoto hiyo kwa ukubwa huo, waifanyie kazi, ili wananchi wapite bila changamoto yoyote katika eneo hilo kwa sababu, katika maeneo yote ambayo tunatekeleza miradi ya barabara au miradi mingine, barabara inapaswa kuwa *passable,* yaani iendelee kupitika wakati huo mradi unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza pia kuhusu uendelezaji wa barabara hiyo. Namkumbusha Mheshimiwa Kaboyoka kwamba, barabara hii yenye kilomita 98 Serikali imekamilisha usanifu mwaka 2018/2019 na ilifanya maamuzi ya kuanza kuijenga 2021 kwa awamu ya kwanza, ambapo zilikuwa ni kilomita 5.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza tunategemea mwishoni mwa mwaka huu, 2025, ikamilike awamu ya pili ya Ndungu – Mkomazi kilomita 36. Tumeshampata mkandarasi ambaye ameanza kufanya kazi na kipande cha tatu cha Same – Mahore, kilomita 56, tupo kwenye hatua ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia mara tu wakandarasi wanapolipwa *advance payment* au fedha za malipo ya awali wanaelekezwa waanze kufanya kazi. Hivyo basi, kwa maeneo yote ambayo wameshalipwa nawaelekeza wakandarasi waanze kufanya kazi mara moja, ili tuweze kuhakikisha miradi hiyo inakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni 12 wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka

Jukwaa la Walimu Wazalendo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jimbo la Ilala. Karibuni.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, Wageni wa Bunge ni viongozi wa Benki ya *CRDB*, Wadau Wakuu wa Bunge Grand Bonanza, Ndugu Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya *CRDB*.

Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Nsekela analitendea haki Taifa letu kwa kweli. Ni kiongozi mwenye utiifu, na uzalendo wako umetukuka. Hongera sana, na Mungu atakujalia utapata makubwa zaidi.

Tunaye Ndugu Tully Mwambapa, Mkurugenzi Mtendaji *CRDB Bank Foundation* na wewe Ndugu Tuli, kazi nzuri unaifanya, lakini tuna kazi yetu pale Ilala. Tulikubaliana jiwe la msingi litawekwa mwezi ujao na anakuja mwenyewe. Nikisema mwenyewe, umeshaelewa, haya sasa kazi kwako.

Tunaye Ndugu Iman Tassama, Msaidizi wa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya *CRDB*; Ndugu Kakuru Katunzi, Mkurugenzi wa Kampuni ya *Cross World Travel Agent* na Mteja Mkubwa wa Benki ya *CRDB*; Ndugu Muhumuliza Buberwa, Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam; Ndugu Iddi Badru, Meneja wa Kanda ya Pwani na Zanzibar; Ndugu Jenipher Tondi, Meneja wa Kanda za Nyanda za Juu; Ndugu Jumanne Wagana, Meneja wa Kanda ya Magharibi; Ndugu Cosmas Saadat, Meneja wa Kanda ya Kaskazini; na Ndugu Chabu Mishwaro, Meneja wa Kanda ya Kati.

Wengine ni wageni 27 wa Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, wanafunzi aliosomanao Shule ya Sekondari Mwenge, Mkoani Singida, wa mwaka 1991 – 1994, karibuni.

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Hawa ni wanafunzi 21 na walimu sita wa Shule ya Msingi *FK International* kutoka Jijini Dar es Salaam.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambaye ni Dkt. Nazar Kirama, Rais wa Shirika la *Internet Society Tanzania* na Mratibu wa Kitaifa wa *Tanzania Internet Governance Forum.*

Wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Umoja wa UKWAMJITA kutoka Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Shangazi, hili jina la Kisambaa au jina gani hili?

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mwalimu Asheri Makasi. Huyu ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam.

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Ester Nicolaus Matiko, Ndugu Annastazia Kirati, Katibu wa Tanzania *Women Chamberof Commerce* kutoka Mkoani Mara. Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, ni Viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Shaurimoyo Zanzibar.

Wengine ni wageni 57 wa Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho ambao ni Kwaya ya Anglikana Dayosisi ya Mara Parish ya Mt. George kutoka Musoma, Mkoa wa Mara.

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, ni Washindi wa Kombe la Mbunge kutoka Malinyi Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Antipas, hongera sana kwa kazi kubwa uliyoifanya kwenye Jimbo lako, na tunawapongeza kwa kushinda kombe hili na Mheshimiwa Mbunge ndio huyu sasa.

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, hawa ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Dodoma na Arusha. Pia wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ni ndugu zake kutoka Peramiho Mkoani Ruvuma na Jijini Dar es Salaam.

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo ni Dkt. Neema Mrimi, Mwenyekiti wa Tawi la Madaktari Chipukizi kutoka Chama cha Madaktari Tanzania. Karibu Dkt. Mussa Mabanda, Daktari wa Huduma za Dharura *TRC*.

Wapo wanafunzi 23 na Walimu watano wa Darasa la Saba kutoka Shule ya Msingi *Pristige* iliyopo Kata ya Bunju, Halmashauri ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam. Wapo pia walimu saba na wanafunzi 93 wa Shule ya Msingi *Mount Everest* ya Mkoani Dar es Salaam.

Tunao viongozi watano wa Taasisi ya Pamoja Tutashinda Tanzania (PATUTA) inayojumuisha wanachama wa Chama cha Mapinduzi, na pia inajihushisha katika kusemea mazuri ya Mheshimiwa Rais kutoka mikoa mbalimbali.

Wafanyabiashara na wajasiriamali 30 kutoka Kariakoo Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Zakayo Shushu. Karibuni sana, ninyi ni wadau muhimu sana kwenye nchi hii na mnalipa kodi vizuri sana. Hongereni. Nikija Dar es Salaam, tutakuwa na kikao na ninyi, kikao maalumu cha kuweka mambo sawa kwenye nchi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, uongozi wa Benki ya *CRDB,* ambao ni wadau wakubwa wa Bunge katika kufanikisha Tamasha la Michezo la *Bunge Grand Bonanza,* wapo Bungeni leo. Nimeshawatambulisha hawa. Sasa nafikiri naendelea.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakumbushwa kuwa bonanza hili litafanyika kesho, Siku ya Jumamosi, Tarehe 21 Juni, 2025 katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlin iliyopo Miyuji Dodoma na itatanguliwa na matembezi yatakayoanza Chuo cha Mipango, Saa 12.00 asubuhi. Aidha, kuanzia saa 12.30 jioni kutakuwa na tafrija itakayofanyika katika viwanja vya Bunge. Waheshimiwa Wabunge na watumishi mnahimizwa kushiriki bonanza hili pamoja na tafrija hiyo bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge linaahirishwa wiki ijayo na kwenye ratiba mimi sitakuwepo kwenye Bunge wiki ijayo. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wote kwa namna tulivyofanya kazi pamoja. *(Makofi)*

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na Mheshimiwa Spika kwa namna nilivyoshirikiana naye na kumtii kwa maelekezo yote aliyotoa. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, bila ninyi mambo haya hayaendi. Naishukuru Serikali, kwa kweli, mmefanya kazi nzuri, kipindi hiki. Tunastahili kujisifia na kujivunia kwenye Taifa letu.

Nawashukuru watendaji, Katibu wa Bunge na timu yake yote, bila wataalam hawa mambo hayaendi, pamoja na wasaidizi wetu ambao wanatembea kilometa zaidi ya 100 kwa siku kwenye Bunge hili.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda majimboni, nendeni na uhakika na ukomavu. Ukishindana na mtu, mshinde kwa mambo mawili; adabu na heshima. Mwache aje na mambo yake, wewe nenda na adabu na heshima. Mwajali watu na hasa wa kipato cha chini, mwaonee huruma hawa, ndio watawapeleka peponi, kwa kujali watu wa chini. *(Makofi)*

Pia, mwajali yatima ambao wanahitaji misaada yetu mingi, ili na wao wawe sehemu ya Taifa letu. Nendeni majimboni na takwimu za kazi alizofanya Mheshimiwa Rais kwenye nchi. Hawa wanaofanya fujo, wanatukana, waacheni wendelee na kutukana, sisi tuna kiongozi nusu mtu, nusu chuma. Daraja la Busisi kalikuta 24%, kaanza nalo, lakini kakabidhiwa lina 24%. Chuma jana kimewekwa, mmekiona kimeng'aa mpaka kwenye *CNN*, kuonesha ujasiri wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Bwawa la Mwalimu Nyerere asilimia tatu, sasa 100%. Haya ndiyo mambo ya kusema. Vituo vya afya, elimu, maji, takwimu; kila mtu awe na takwimu yake, achukue kabisa takwimu. Kama hamna, nendeni kwa Waheshimiwa Mawaziri watawapa ili muweze kuwaambia wananchi kitu gani Mheshimiwa Rais, Mama Samia, kafanya kwenye nchi, yeye achaguliwe, wewe

uchaguliwe, na Diwani achaguliwe. Tunakwenda na mafiga haya matatu. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo machache, nimechomekea tu jamani leo, maana yake ukipata fursa ndiyo naitumia hapo hapo. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa upendo na utiifu, lakini nawashukuru wananchi wa Jimbo la Ilala, kwa kweli, nimewaheshimu, nimewaenzi, nimewajali, nimejituma kwao kwa hali na mali kuhakikisha tunaishi pamoja, tunavuka pamoja na tunakwenda pamoja. Nawashukuru wananchi. *(Makofi)*

Nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi, Wilaya ya Ilala, chini ya Mwenyekiti Saidi Side na Katibu, Chifu Yeredi, kwa namna walivyoishika wilaya na CCM kwenye Wilaya ya Ilala. Mheshimiwa Mama Samia ajue kazi zinafanywa na yeye atapata ushindi mkubwa sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tuna wachangiaji wa kutosha. Nimwite sasa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa

Asia Abdulkarimu Halamga, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hizi mbili ambazo ziko Mezani kwetu. Nianze kwa kuwapongeza hawa Mawaziri wawili; Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango na Uwekezaji pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mawaziri hawa ni wachapakazi, ni wasikivu, wanafikika, na kila muda wapo tayari kurekebisha mipango yao ili kusikiliza mahitaji ya watu, lakini pia wana bahati ya kupewa wasaidizi ambao nao ni wasikivu vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Chande, ni Naibu Waziri msikivu, mnyenyekevu na muda wote yupo tayari kusikiliza kero za sisi Wabunge. Vilevile kaka yangu Stanslaus Nyongo ni Mbunge mahiri, mchapakazi. Hata alipoteuliwa kuwa Waziri, hajapandisha mabega juu. Bado tunaye tunatamba naye na tunashirikiana naye. Kwa hiyo, hongereni sana Mawaziri na Manaibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake mapana na jinsi anavyoendelea kuchapa kazi na kutusaidia sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jana tu tumeshuhudia kazi kubwa ikitendeka, na Afrika Mashariki jana ilizizima tulipokuwa tunashuhudia uzinduzi wa Daraja la Busisi. Kama alivyosema hapo Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alikuta daraja hili limetekelezwa kwa 24%, lakini kwa maono yake, kwa ujasiri wake ametekeleza kwa 100%. Hongera sana Mheshimiwa Rais. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema na umri mrefu ili tuendelee kunufaika na busara zake na uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu katika maeneo matatu. Sehemu ya kwanza ni kuhusu sekta ndogo ya

korosho. Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa inayoifanya katika uwekezaji wa sekta hii ndogo ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia miaka minne mfululizo wakulima wa korosho wakipata pembejeo kwa ruzuku ya 100%. Tumeshuhudia pia Mheshimiwa Rais anafanya maamuzi magumu kwa kutoa 100% ya *Export Levy,* kwamba yote ipelekwe kwenye tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, msimu huu Wizara ya Kilimo na Bodi ya Korosho imeajiri Maafisa Ugani 500 ili kwenda chini kuwasaidia wakulima wa korosho. Siyo hivyo tu, tumeshuhudia msimu uliopita kwamba minada yetu imeendeshwa kidigitali kupitia *TMX*. Kwa hiyo, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais, uwekezaji wake tunauona katika sekta ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina mambo mawili tu ya kushauri. Kazi hii nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais, matunda yake yanaanza kuonekana. Kwa mfano, usambazaji wa pembejeo kwa 100%, mwaka 2024 kulikuwa na ongezeko kubwa sana la uzalishaji wa korosho. Tumetoka tani 315,000 na tumefikia tani 525,000 Kitaifa. Hata hivyo, takwimu hizi haziendi sambamba na ongezeko la ubanguaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Serikali sasa ifanye mipango wa kuwa na mpango na vivutio maalum wa kuhakikisha sasa tunatoa kipaumbele kwa wabanguaji wetu wa ndani ili tulinde ajira za wanawake na vijana. Si hivyo tu, ni pamoja na kuongezea thamani korosho yetu ambayo itakwenda kupata bei nzuri huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bei ambayo tumeipata miaka miwili hapa nchini kwetu inawezekana ni kwa sababu wenzetu wazalishaji wa korosho Afrika Magharibi wameamua kuzuia korosho yao isiuzwe nje ikiwa korosho ghafi, wanabangua. Kwa mfano *Benin, Ivory Coast* wamefanya hivyo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali yetu ijikite sasa ili na sisi tuwe na mipango ya kuhakikisha kwamba ubanguaji unafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa hatua nzuri ambazo imeanza kuzichukua. Tuna kongani ya Kiwanda cha Korosho pale Malanje. Kama tulivyoona kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka huu, kuna mwekezaji amepatikana, atabangua tani 100. Hiyo ni hatua nzuri, tunataka wabanguaji wengine wapatikane ili korosho yetu yote tubangue ndani na tupeleke nje korosho na karanga ili wakulima wetu wanufaike na mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mwaka 2024 tumeshuhudia uchache au upungufu wa maghala baada ya uzalishaji kuongezeka. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke mpango maalum wa kujenga maghala katika maeneo yetu, tusiwe na maghala ya wilaya tu, twende hadi kwenye ngazi ya tarafa ili tuhakikishe kwamba korosho ikitoka kwa mkulima iende ghalani siku ya tatu iende mnadani na hatimaye mkulima, korosho yake ifike mnadani mapema na apate bei ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeshauri Wizara, Bodi ya Korosho na vyama vikuu vya ushirika watengeneze mpango wa kuongeza maghala katika maeneo yetu. Mimi ningeshauri kwenye Jimbo langu la Nanyamba, tungeweza kuweka ghala pale Kiromba, tungeweza kuweka ghala pale maeneo ya Hinju na maghala makubwa tukaweka pale Nanyamba Mjini ili kuhakikisha kwamba korosho ikitoka kwa mkulima inapokelewa, na baada ya siku chache inakwenda mnadani na siyo kama tulivyoshuhudia mwaka 2024, tulipoona korosho yetu inaloana na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho ikiathirika na mvua hata ubora wake unaathirika na hatimaye kupata bei ambayo ni ndogo inapopelekwa mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ulikuwa ni kuhusu *Mtwara Corridor. Mtwara corridor* ni mpango ambao ulianzishwa huko nyuma na viongozi wetu wa Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia; na lengo lake kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Bandari yetu ya Mtwara inaunganishwa na barabara,

reli na usafiri wa maji; na kukawa na mipango mizuri sana ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuubeba mpango huu sasa na kuanza kuutekeleza. Tumeshuhudia sasa Barabara ya Uchumi kutoka Mtwara Nanyamba - Newala mpaka Masasi inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna maboresho makubwa yanafanyika katika Barabara yetu ya Mingoyo - Mtwara na Mingoyo – Masasi. Sasa hivi tumeona kwenye mpango wetu kwamba tuna ujenzi wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hili suala la ujenzi wa reli ya Mtwara hadi Mbamba Bay sasa tuutekeleze, tuongeze kasi ya utekelezaji na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga. Wananchi wa maeneo hayo wanasubiri sana mradi huo ili uboreshe maeneo yetu na hatimaye Bandari yetu ya Mtwara iweze kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, tutakuwa tumeifungua Mtwara, tutakuwa tumeifungua Lindi na vilevile Liganga na Mchuchuma, sasa chuma kitakuwa kimepata sehemu ya kusafirisha. Siyo hivyo tu, tutapata mzigo kutoka nchi za Malawi, Msumbiji, na Zambia ili ipelekwe kwenye Bandari yetu ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana kwamba sasa uwe muda wa utekelezaji wa mradi huu, ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho ni kuhusiana na sekta ndogo ya gesi. Ninaipongeza Wizara na Shirika la *TPDC* kwa kazi nzuri ambayo inafanywa. Vilevile ninaipongeza Serikali kwa kuamua sasa kufanya mashauriano na wale wawekezaji ili mradi wetu wa *LNG* uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwamba kwa kipindi kilichobaki sasa hivi tuongeze kasi ya mashauriano, tuongeze kasi ya majadiliano ili mradi utekelezwe. Wenzetu wa Msumbiji majirani zetu wanaekwenda kwa kasi sana. Ni muda mwafaka sasa na sisi twende kwa kasi ili gesi yetu ya Mtwara, na gesi yetu ya Lindi iweze kuchakatwa pale Likong'o Lindi na hatimaye tupate fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninashauri kwamba kasi ya mashauriano iongezwe. Vilevile kupitia *TPDC* tuongeze kasi ya kuongeza vituo vya *CNG* ili gari zetu ziweze kutumia hiyo gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna mradi wa kusambaza gesi asilia nyumbani. Tumeanza Lindi na Mtwara, lakini kaya ambazo zimenufaika ni chache sana. Ni muda mwafaka wa kutenga fedha za kutosha ili gesi hiyo isambazwe, siyo Mtwara na Lindi pekee, kuwe na *line* mbalimbali. Twende hadi Masasi, iende Tunduru mpaka Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuwe na *route* nyingine ambayo inaenda mpaka Dar es Salaam na maeneo mengine. Taasisi za umma zipewe kipaumbele, vilevile hospitali za umma zipewe kipaumbele, na maeneo mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha usambazaji wa gesi hii asilia nyumbani, sasa hivi kasi yake ni ndogo sana. Sababu kubwa ni kwamba hazijatengwa fedha za kutosha kwa ajili ya mradi huo. Ninaiomba Serikali, naiomba Wizara na kupitia *TPDC* fedha za kutosha zitengwe ili gesi hii ipelekwe nyumbani na hatimaye Serikali ipate fedha za kutosha, na vilevile ili wananchi wetu wanufaike na gesi yao ambayo ipo ya kutosha kwa maeneo ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu sisi Wanananyamba, hatumdai Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatudai yeye, na tumejiandaa kwamba mwezi Oktoba tunatiki na tuna kapu kubwa la kura zake ambazo tayari tumeziandaa kwa ajili ya kujaza kura kwa ajili ya Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota, nilimwita Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuata, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ajiandae. Simuoni Mheshimiwa Halamga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kama yuko tayari.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali pamoja na Wizara ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuweza kunipa uhai na kusimama leo mbele ya Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukiwa tunakaribia kuvunja Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba Mwenyezi Mungu anisaidie na awasaidie Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wote ambao wameifanya kazi hii kwa weledi mkubwa ndani ya miaka mitano, kwa kuhakikisha kwamba wanamsaidia au tunamsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendesha mambo yake kwa weledi na kwa umakini mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yamefanya tuendelee kutambulika na kufahamika kote ulimwenguni, ni kwa ajili ya umahiri wa Mama huyu mwanamke hodari, mwanamke shupavu, mwanamke mwenye maono, mwanamke mwenye malengo ambaye ndiye ametufikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kokote Tanzania inaposimama leo hii, haiachi kumteua au kumchagua mtu yeyote kuhakikisha kwamba anasimama kwa niaba ya Taifa letu la Tanzania. Aliyeyatengeneza haya sio mwingine bali ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hongera sana mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo na kutoa shukurani kwa Mungu, ninaomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amemwaga fedha kona zote za Taifa letu la Tanzania, kuanzia mijini hadi vitongojini. Ndiyo maana Mbunge yeyote atakayesimama katika Bunge hili hawezi kuacha kumpongeza, hata wale ambao walikuwa hawajaona maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine walikuwa hawajaona maji ya bomba katika Taifa hili, lakini leo watu wameona maji ya bomba, wameona umeme, wameona barabara nzuri, wameona vituo vya afya, wameona huduma za jamii za kila aina, zikionekana katika Taifa letu la Tanzania. Sio mwingine bali ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwamba mama amemwaga fedha nyingi sana kwa sababu mimi mwenyewe nikiwa ni shahidi juu ya mambo hayo, amemwaga kwenye barabara; kwa mfano Jimbo langu tu la Mchinga ametuletea shilingi bilioni 11; kwenye maji, shilingi bilioni 18; afya, usiseme; nishati, amehakikisha kwamba vijiji vyote vya Jimbo la Mchinga vimepata nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Jimbo la Mchinga lina vitongoji 236. Kati ya vitongoji hivyo 181 leo hii vinawaka umeme na ni maendeleo, kwani bila umeme hakuna maendeleo. Kwenye elimu ametoa shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndicho yeye amekipa umuhimu mkubwa katika Taifa letu. Bila chakula hakuna kitu. Kila mwanadamu anategemea chakula. Leo hii kwenye kilimo ametuwekea shilingi bilioni 31.3. Hii tangu anaanza kulihutubia Bunge letu, hili aliweka kipaumbele kwenye kilimo, na ndiyo maana bajeti ya kilimo ilitoka kwenye shilingi milioni 290 kule, ikaja mpaka trilioni. Hii yote ni kazi ya Mama Samia Suluhu Hassan na

ndiyo maana leo ninaposimama kuzungumza, nina kila sababu ya kumpongeza kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo sasa hivi tumekuwa wa pili barani Afrika kwa uzalishaji. Haya yote ni kwa ajili ya maono mazuri ambayo ameyaonyesha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hongera sana Mama. Tuna kazi kubwa; na siyo kubwa, tarehe ikifika tunachukua, tunaweka, waaa! Kwa nani? Kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Makamu wa Rais, amekuwa ni msaidizi mzuri sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yeye ndiye aliyekuwa msimamizi mzuri wa Shughuli za Serikali Bungeni. Bila kusimamia vizuri Shughuli za Serikali Bungeni, wakati mwingine kuna baadhi ya mambo yanaweza yasiende sawa, lakini kila jambo liliweza kwenda vizuri. Ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa uwasilishaji wako mzuri wa bajeti yetu ambayo ni bajeti inayojipambanua kwa kila eneo, pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wa Wizara, na watendaji wote, bila kumsahau Profesa ambaye yuko pembeni yake ambaye wao wenyewe wanaitana kaka mdogo, kaka mkubwa. Waendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaweka wao; amejua jinsi wanavyoweza kuchapa kazi, na akaona hakuna matata. Kazi hii wanaiweza vijana kutoka Singida. Hongera sana kwa vijana wa Singida, Mama anawaamini na anawapenda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya kazi kubwa na nzuri katika kuliongoza Bunge. Kazi aliyoifanya katika kuliongoza Bunge hili pamoja na Naibu Spika ni kazi zenye viwango, na kila mtu

anaziona kazi hizo. Hongereni sana; na wakisaidiwa na Wenyeviti wao, wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wewe Mwenyekiti Mwanyika ambaye ni Mwenyekiti wangu katika Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, hongera sana, umefanya kazi nzuri. Tunaamini tunamaliza hili Bunge, tutarudi huko majimboni, na tukirudi majimboni kwa kazi hizi zilizofanyika, hakuna mtu atakayesema, huyu hawezi. Wote tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, uongozi ni wote. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba hapa au Mama Samia Suluhu Hassan ana mwenza wake na hata sisi Wabunge tuna wenza wetu. Tunawapongeza sana Wabunge hawa wenza wa Wabunge; mwenza wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba anamsaidia kwa hali na mali, na mambo yake yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie, Mama Samia ni Rais. Pamoja na Urais wake, anazungukwa na walinzi chungu nzima, lakini ikifika usiku anaenda kulala. Akishaenda kulala, kwanza anamtegemea Mungu, na mwenza wake ndiye anayeweza kumfariji, hata kama akiwa na misongo ile, mwenzi ndiye mtu wa kwanza kumpa faraja. Bila yeye mambo hayaendi vizuri. Hongereni sana wenza wa viongozi, na hongereni sana wenza wa Wabunge kwa kusaidiana na Wabunge hawa. Endeleeni kufanya hivyo, tunawategemea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka nije kwenye kilimo. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Mama amefanya kazi kubwa kuongeza bajeti, na ndiyo maana kilimo kimepanda kupita kiasi. Leo Tanzania inategemewa na Afrika katika suala zima la kilimo. Sasa Mama amehimiza kilimo, na watu wamelima vizuri na wamelima kwa bidii. Korosho wamelima sana, ufuta wamelima sana kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kutokana na changamoto zilizojitokeza, juzi tulikuwa na mnada wa ufuta. Ufuta ulipanda mpaka shilingi 4,000.00. Sasa hivi bei ya ufuta kwa ule

mnada wa kwanza imeshuka mpaka shilingi 2,700.00. Nini ninachotaka kusema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitegemee soko moja, pamoja na kwamba ninajua Serikali inafanya kazi kubwa na nzuri ya kutafuta masoko, tuendelee kutafuta masoko ili wananchi hawa waliojitokeza na waliojipambanua kulima kwa bidii, juhudi na maarifa, itakapofika wakati wauze mazao yao kwa bei ambayo itakuwa ni nzuri na wataifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni barabara. Mimi kwangu kule tunalima ufuta. Ninamwomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, yeye ndiye Waziri wa Fedha, kule wamelima ufuta lakini hauwezi kutoka Mipingo kuja hapa kwenye maghala, wala hauwezi kufika pale Mkwajuni. Ninaomba anisaidie fedha ili waweze kuleta ule ufuta kwenye vituo vya kuuzia. Mheshimiwa tafadhali ninakuomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye afya, tumepunguza tozo kuhusu vileo ili kuleta ushindani. Kuna kitu kinaitwa *energy*. *Energy* ni shida, na ni tatizo. *Energy* inauzwa madukani na wanaokunywa ni watoto wadogo. Wanakunywa *energy* kwa malengo yapi? Kama wanaweza sasa hivi umri wa miaka 13 ku-*boost* ile nguvu ije, wakifika umri wa miaka 28 watakuwa katika hali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *energy* jamani zinaharibu hao watoto. Tutengeneze kitu mbadala. Tuweke mikakati ya kupunguza haya ma-*energy*. Ni hatari, watoto wanaangamia. Tunategemea vijana ndio wanaotutegemea sisi baada ya kuondoka, vinginevyo ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa 100%, na ninawatakia Wabunge wenzangu kila la heri. Ninaamini wote tutashinda. Ninawashukuru sana wapigakura wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Mkoa wangu wa Lindi. Ninawashukuru wote, ninaamini sote tutarudi.

Ninawashukuru sana Wanamchinga kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru ninyi viongozi wote, Wabunge, watumishi na wasiokuwa watumishi kwa ushirikiano mkubwa mlionipa. Mungu awabariki, *inshallah* tutarudi tena Bunge lijalo. Sina mashaka hata kidogo tutarudi sote humu Bunge lijalo kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa muda huu, nawe Mwenyezi Mungu atakurudisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Amina. Ahsante sana Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mwenza wa Rais wetu wa Awamu ya Nne.

Nilimwita Dkt. Thea Medard Ntara atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, na Mheshimiwa Athuman Almas Maige ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuweza kukaa ndani ya Bunge hili kwa miaka mitano. Ninamshukuru sana Mungu kwamba ametupa afya, lakini pia tuwaombee wale wote ambao walituacha kipindi hiki, basi Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema Peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru sana Wabunge ambao ni Mawaziri; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Chande wanafanya kazi nzuri. Wanapiga kazi nzuri. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anajua hiyo Wizara ni nyeti, lazima kutakuwa na mawe kila kona, lakini akaze mwendo na aendelee. Ninajua tunamaliza Bunge, lakini Serikali bado ipo. Kwa hiyo, mawaziri bado tunawategemea watafanya kazi katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na eneo la elimu. Kwanza, ninapongeza sana, kuna maeneo makuu mawili ambayo yamefanyiwa kazi kipindi cha miaka mitano. Moja ni la mikopo.

Tulikuwa na mikopo kama shilingi bilioni 464, lakini mpaka sasa ikapanda kufikia shilingi bilioni 787.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, suala la mikopo mnajua lilikuwa na kelele miaka miwili iliyopita, lakini tuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, mikopo hii ilivyoongezeka, kelele ziliisha. Niwaambie, vyuo vikuu vilitulia. Vurugu hakuna vyuo vikuu. Wahadhiri pia walitulia, ingawa wana changamoto kidogo nitazisema, lakini mikopo imefanya vyuo vikuu vimetulia, na niseme Serikali ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ni muhimu katika elimu lililofanywa ni uboreshaji wa mitaala. Mheshimiwa Rais alipotoa yale maagizo kwamba mitaala iboreshwe na imefanyika hivyo, niseme Waheshimiwa Wabunge baada ya miaka 10 wanafunzi wetu hao, vijana wetu wataweza kujiajiri kwa sababu ya lile eneo la amali. Kwa hiyo, hata kelele za ajira zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa lililofanyika katika kipindi hiki kubadilisha mitaala na ilikuwa ni nguvu ya Rais kusema kwamba ninataka mkarudie, hebu mfanye *review,* rudieni mitaala, mwone kwamba tunaifanya vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tulikuwa tunalalamika humu ndani kwamba elimu yetu haitusaidii. Kwa hiyo, suala la mitaala ni muhimu sana, na ninampongeza sana Rais kwamba aliliona hilo na akaona ni muhimu mitaala hiyo ibadilishwe. Kwa hiyo, uboreshaji wa mitaala utaleta ajira baada ya miaka 10. Tuvute subira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine sasa nije kwenye maombi kwa huo upande wa elimu. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nimefurahi sana kwamba yupo hapo. Suala la madeni ninamwombe sana sana Mheshimiwa Waziri chonde chonde, mimi ninapenda bado nirudi kuwa mwakilishi wa vyuo vikuu. Ningekuwa hapo karibu labda ningempigia magoti au ningegaragara kama wanavyofanya Wangoni, nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu

madeni ya wahadhiri na wafanyakazi wa vyuo vikuu, hebu wamalizane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, pale Chuo cha Ushirika wanadai shilingi bilioni 1.1 lakini ukienda *SUA* wana madeni, ukienda *UDOM* wana madeni, na ukienda *Open University* wana madeni. Hebu tumalizane nao hawa watu. Wanafanya kazi kwa utulivu, hutaweza kusikia sijui kuna migogoro au wanagomagoma. Ninamwona Mheshimiwa Waziri anaandika hapo. Ninakushukuru, akalifanyie kazi hilo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali kwa ujumla ikaangalie sana *retirement age*. Bado wahadhiri wanalalamika hasa maprofesa. Vyuo vyetu nimekwambia mara nyingi hakuna maprofesa.

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tulikuwa sote pale chuoni wakati wewe unasoma *Ph.D,* tunagongana gongana kwenye *corridor*. Maprofesa ni wachache mno. Unapishana tu na ma-*Assistant Lecturer. Retirement age* mwiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu ninaamini Waziri wa Utumishi yupo, Mheshimiwa Simbachawene ananisikia. Tuangalie *retirement age* ya wahadhiri. Ubongo hauzeeki haraka. Mtu akiwa profesa au daktari kule chuo kikuu hubebi mizigo, hubebi matofali kule, ni akili tu inafanya kazi. Kwa hiyo, niwaombe mwangalie *retirement age* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa upande wa elimu, wenzangu waliongea. Ninawaomba sana tuangalie namna gani tunaondoa kuamsha saa 10 ya usiku watoto wa chekechea mpaka darasa la tatu. Tufanye kama wenzetu. Korea na Japan wanaanza masomo saa tatu, mbona wanafanya vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watoto wadogo kuwabeba saa 10 ya usiku kwenye magari; nimelisema hilo na mwenzangu alilisema, ninafikiri ni Mheshimiwa Neema. Niwaombe jamani hili tuliangalie litatuletea balaa. Tuangalie kabisa hawa watoto wadogo wanaosoma, wapelekwe shuleni kuanzia saa moja na

nusu, lakini siyo saa 12. Wenye shule wanapenda wao wanawabeba tu kwenye magari lakini waangalie na akili ya watoto. Hilo ninaona nimelimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la afya. Mimi niombe, kuna tatizo kubwa sana la ugumba. Kuna wanawake wengi wanashindwa kupata watoto. Ninaomba Hospitali ya Benjamin pamoja na Hospitali ya Muhimbili waboreshe kitengo kile cha *IVF,* wanawake wasaidiwe. Kwenda kupandikiza watoto jamani ni gharama kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanawake wanaopata hilo tatizo linawa-*affect* mpaka kwenye ubongo. Akili yao haiko sawa. Tuwasaidie, tunaposema *family planning,* tuiingize huko. Hata kuwasaidia hawa, tena ikibidi bure. Kupandikiza mtoto ni shilingi milioni 15 au milioni 20, hawawezi. Waziri wa Afya akaliangalie hilo, upandikizaji wa watoto uwe bure au walipe fedha ndogo sana. Hili jambo tunaliona tu dogo, lakini sasa hivi ni suala kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wanaume wanaona aibu kwenda hospitali na kusema mimi sizai. Kwa hiyo, hospitali iweke kitengo kitakachoweza kushirikisha wote: wanaume na wanawake ili mtu aweze kupata mtoto. Kutokupata mtoto ni umaskini kama umaskini mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri nizungumze kuhusu ardhi. Mimi ninatoa tu maoni yangu kuhusu ardhi. Jamani Wizara ya Ardhi hebu ilete *programme* ya kuondoa nyumba zote za nyasi na nyumba zote za matope. Wakipanga hiyo *programme,* wanaweza kuwaambia wananchi kwamba, kila mwananchi afyatue matofali, ajenge nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakusanya fedha kutoka kwenye zao la tumbaku, na madini. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atafute fedha, watu wa namna hiyo wanaambiwa jenga nyumba nzuri, Serikali pelekeni mabati. Ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa ninaangalia takwimu, yaani tumefikia wakati takwimu mikoa ambayo inaongoza kwa nyumba ambazo siyo bora; ninaomba mnisikilize. Lindi, Tabora, Mtwara, Ruvuma, na Rukwa. Sasa mpaka mimi ninashangaa. Mtwara wanalima korosho, sasa mjue kwa nini wananchi wa kule nyumba zao bado ni za nyasi. Ruvuma ninajua wilaya zinazotuangusha kule, ninazifahamu, Namtumbo ni mojawapo, pamoja na Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nyumba za nyasi mpaka leo, halafu nyumba zinazoezekwa kwa udongo Singida, na Dodoma; Singida ni kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Hebu tuwasaidie. Tupeleke bati tuwahamasishe nyumba za matofali…

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, peleka bati.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba Singida sasa hakuna nyumba ya tembe hata moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Amandus Chinguile, unaipokea?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Nimepita huko, ila sasa ndiyo hivyo Mheshimiwa Mbunge si anaona aibu; lakini Singida, Dodoma, Manyara, Shinyanga, na Simiyu, tuwapongeze wale ambao mikoa yao hakuna nyumba za nyasi. Mkoa unaoongoza ni wa Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Njombe ni bati tupu; Kilimanjaro bati, Dar es Salaam na hata

Kagera pamoja na Katavi. Tena mpaka nimeshangaa hata Katavi kumbe wako juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni kampeni inaweza ikafanyika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tuondoe hili. Tafuta fedha kila mahali. Mwone Waziri wa Madini wakupe fedha, ziko kule. Waziri wa Kilimo anasema anapata fedha nyingi za kigeni kutoka kwenye tumbaku, mbane alete hizo fedha wananchi hawa wapate bati.

La mwisho, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu leo ndiyo unisaidie hili la mwisho. Ninaomba sana, nilikuomba sana kuhusu wale ma-*DC* na ma-*RC*. Hebu uende ukaongee na mkuu wa nchi, wapate ile *HS*. Andika hapo. Wapate ile *HS,* Wakuu wa Wilaya wanalalamika mno. Tumalizane nao lile deni wanaita *hand shake* Mheshimiwa Kikwete alisaini. Sasa ninakuomba ukamalize na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Basi nilimwita Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia, ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa afya njema ili niweze kuongea katika Bunge lako Tukufu katika kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, Hoja ya Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ninaomba kuunga mkono maoni ya Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamezungumza kuendelea kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya maendeleo ambayo amekuwa akiifanya kwa ajili yetu sisi Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo liko wazi kabisa dhahiri shahiri, mwenye macho haambiwi tazama; mwenye kusikia haambiwi sikia; na mwenye kugusa haambiwi gusa; yaani ile milango yote ya fahamu ambayo binadamu anayo inabaini na kutambua kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ninaomba niwapongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa kwa ajili ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imetekelezwa imebainishwa katika ukurasa wa 14 wa hotuba hii. Ninatambua Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetekeleza miradi mbalimbali kwa fedha nyingi sana, matrilioni na matrilioni kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika mkoa wangu wa Dodoma, ambao ndiyo Makao Makuu ya nchi hii ya Tanzania. Miaka 10 iliyopita ninaamini wengi wetu ni mashahidi, Dodoma iliyopo sasa siyo ile ya miaka 10 iliyopita. Kwa hiyo, ninaendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ya maendeleo ambayo tumeyapata katika Mkoa wetu wa Dodoma. Miongoni mwao, ninaomba niseme kwamba Serikali imetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 3,093. Hili siyo jambo dogo kwa ajili ya maendeleo ya Wanadodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanadodoma, tuna kila sababu ya kuendelea kumshukuru, lakini pia kumwombea Mwenyezi Mungu, awe na afya njema, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba Mwenyezi Mungu akitujalia afya na uhai mwezi Oktoba tuhakikishe tunampa kura za *Tsunami* kwamba Dodoma ameipendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikibainisha tu baadhi ya miradi ni pamoja na ujenzi wa barabara ya mzunguko ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 221, na hivi juzi tulifanya ziara ya kuikagua na

yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tunaendelea kuishukuru sana kwa sababu ujenzi wa mradi huu una maana kwamba utapunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dodoma. Pongezi sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Msalato. Tunatambua kabisa kwamba huu utakuwa ni uwanja wa Kimataifa. Hivyo, ndege za kuingia na kutoka Mataifa mbalimbali zitafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo mradi wa uwekezaji mfumo wa umeme chini ya ardhi katika Mji wa Serikali ambao thamani yake ni shilingi bilioni 50.99. Pia ujenzi wa Mji wa Serikali ambao ni kivutio kikubwa sana katika Mji wetu wa Dodoma. Mwisho wa siku mimi naamini na kuna watu wanaweza wakajitokeza kwenda kufanya utalii katika eneo lile kwa jinsi ulivyojengwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwenye suala zima la huduma za kijamii ikiwemo elimu na afya, lakini nijikite zaidi kwenye elimu. Naendelea kuipongeza Serikali kwa kuwa na miradi mbalimbali ya kuhakikisha kwamba elimu pia inapewa kipaumbele kwa kujengwa miundombinu sahihi ili kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naomba niseme wazi, dhahiri, shahiri kwamba, Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa wanufaika wakubwa sana wa ujenzi wa miundombinu hii, na hii imesaidia kuchagiza kwamba, yale mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia imefanya Mkoa wetu wa Dodoma uwe miongoni mwa mikoa ambayo imefanya vizuri sana katika mitihani ya Kitaifa na kuwa mkoa wa nne, hili siyo jambo dogo. Kwa hiyo, tunaendelea sana kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha kwamba miradi ya kimaendeleo inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nitoe ushauri kwamba, basi Serikali ione umuhimu wa kujenga nyumba za walimu katika shule zote, za sekondari pamoja na shule za msingi ili kuwawezesha hawa walimu nao kuwa katika mazingira

bora ya utendaji kazi ili mwisho wa siku mafanikio zaidi katika suala la elimu yaweze kupatikana na hatimaye tupate wataalam mbalimbali kutoka katika shule hizo ambazo walimu wao wanawafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nizungumzie suala zima la mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Mkoa wa Dodoma umekuwa ni miongoni mwa mikoa ambayo pia imefaidika na uwekezaji mkubwa sana ambao pia uwekezaji huu utasaidia kwanza, kupata ajira kwa wananchi wa Dodoma; kuongeza kodi pamoja na kipato kwa ajili ya wananchi wa Dodoma. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji pamoja na ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Dodoma tunajivunia viwanda mbalimbali vya usindikaji ikiwemo Kiwanda cha Mafuta cha *Mainland* cha kusindika mafuta ya alizeti ambacho kimekuwa kikisindika mafuta tani 250 kwa siku. Hili siyo jambo dogo. Hii maana yake nini? Ni kwamba tukiwa na viwanda vingi zaidi itasaidia kutokuagiza mafuta kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mkoa wa Dodoma tunalima sana zao la karanga, na kwa sababu hiyo, nilikuwa natamani niendelee kuishauri Serikali kuona namna bora ya kuboresha zile mbegu za karanga ili tuweze kuzalisha karanga nyingi na hatimaye tuweze kupata viwanda vya kusindika mafuta ya karanga, nayo pia itasaidia katika kuhakikisha upungufu wa mafuta unapungua nchini badala ya kutegemea kuagiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia tuna viwanda vya madini ya shaba ambayo pia inaongeza thamani. Pia ukitaka viatu Dodoma, tuna viwanda. Tuna kiwanda cha Jin'kui ambacho kiko kule Zuzu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mjue kwamba Dodoma sasa hivi ina viwanda vya kutosha. Ukweli ni kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameufanyia

mambo mengi kabisa Mkoa wa Dodoma, na ninaamini na sisi hatutamwangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusiana na mapato ya ndani, kwamba, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba, mapato ya ndani yamepanda kutoka shilingi trilioni 20.95 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 29.83. Hili siyo jambo dogo. Kwa hiyo, tuendelee tu kuiomba Wizara iendelee kuhamasisha wananchi waweze kudai risiti na wafanyabiashara waweze kutoa risiti ili kusudi tuweze kupata mapato ya kutosha na hatimaye kodi hii itumike kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, badala ya kutegemea wafadhili au kutegemea ufadhili kutoka nje ambapo mwisho wa siku wakiamua kukata ufadhili wao, inakuwa ni mtihani kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, naomba niendelee kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Pia, naomba niwashukuru na waume zao, kwa sababu kama hao waume zao wasingewaruhusu kuja kunichagua, maana yake nisingepata nafasi hii. Kwa hiyo, naomba niwashukuru wote na nitaendelea kuwasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba tena niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi wote kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya. Hakika mwenye macho haambiwi tazama. Sisi wananchi wa Dodoma tunamwahidi, sisi tuna deni na Waswahili wanasema, "dawa ya deni ni kulipa," na deni hilo tutalipa mwezi Oktoba kwa kumpa kura za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. Nilimwita Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuata, na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya Bajeti Kuu ya ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Wizara ya Fedha, na pia Wizara ya Mipango kwa mwaka huu 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kujiunga na wachangiaji wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa, nina afya nzuri baada ya miaka mitano kutumikia Bunge hili na kuwatumikia waliotupigia kura kutuleta humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na kutoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mengi aliyotufanyia. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwetu Jimbo la Uyui tunamwona kila siku kwa alama alizoziweka. Naweza kuzitaja hapa alama hizo ambazo pia wenzangu mkumbuke kuhusu pongezi hizi tunazozitoa kwa Mheshimiwa Rais. Kwanza, ni afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza, hatukuwa hata na kituo kimoja cha afya, tunamaliza na vituo vinne vya afya katika Jimbo langu, lakini hatukuwa na hospitali ya Wilaya; Mama Samia ametujengea hospitali mpya ya Wilaya, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumejenga zahanati nane mpya katika kipindi cha uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan. Haya siyo mambo madogo kwa Wanauyui. Kuhusu maji, Jimbo la Tabora Kaskazini zamani, siku hizi linaitwa Uyui, lina vijiji 58 vinatumia maji ya Ziwa Victoria, lakini tuna vijiji 98, na vijiji 71 vina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa miji 28 kujengwa, maji yakienda Urambo yatatitirika maji katika Jimbo la Uyui na hivyo vijiji zaidi 72 kwa ujumla vitapata maji, na hii itakuwa zaidi ya 89% ya vijiji vyote kupata maji katika Jimbo la Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tulipoanza kulikuwa na Kata zaidi ya 10 hazina sekondari, leo Kata zote 19 za Jimbo la Tabora Kaskazini zamani, siku hizi Jimbo la Uyui, zina sekondari na

nina sekondari moja imebaki ya ziada naipeleka katika Kata ya Mabama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumejengewa Kituo cha *VETA* ambacho hakikuwepo. Tumejengewa shule za upili wa juu, yaani *form five* na *form six* tatu, na tumejengewa shule za msingi moja lakini tumekarabati shule nyingi, madarasa mengi, tuna madarasa mengi sasa kuliko idadi ya wanafunzi. Tuna tatizo dogo tu la madawati ambalo tumejitahidi kuyajengea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la nyumba ambalo nililisemea ndani ya Bunge, Serikali inisaidie kujenga nyumba kwenye bajeti inayokuja, nimeziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme. Jimbo la Uyui vijiji vyote 98 vina umeme, na vitongoji 15 vina umeme; na juzi Naibu Waziri hapa amenipa orodha ya vitongoji 86, vingine vitapata umeme katika Jimbo la Tabora Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, kulikuwa kuna matatizo ya ruzuku. Tuna ruzuku ya mbolea, na mbolea ya ruzuku. Ruzuku ya mbolea ilikuwa ya msimu uliopita. Serikali ya Mama Samia ilijitolea kuwalipa wananchi walionunua pembejeo kwa bei kamili, akawalipa ruzuku na tumeanza kulipa. Wamebakia watu wachache ambao hawajalipwa, lakini tunaendelea kulipa. Mwaka huu pembejeo zote zinanunuliwa kwa bei nusu. Serikali imelipa nusu, pongezi sana kwa Mheshimiwa Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tumbaku, Jimbo la Tabora Uyui huwezi kuongelea chochote kuhusu biashara bila kutaja neno la tumbaku ambalo Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara analipiga vita; lakini tumbaku tumeilima miaka mingi na ni zao la biashara kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na matatizo makubwa sana miaka mitano iliyopita. Tulikuwa hatuna wanunuzi, leo tuna wanunuzi 12 wa tumbaku. Ilikuwa huwezi kulima tumbaku mpaka upewe mgao. Sasa tunalima tumbaku kwa nguvu yetu. Hongera

sana kwa Mheshimiwa Waziri Bashe na hongera sana kwa Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora. Halmashauri ya Uyui ilikuwa haina majengo, tumejengewa majengo mapya pamoja na ukumbi mpya; pia tunajengewa Mahakama. Kwa muda huu wa Mama Samia Suluhu Hassan, tunampongeza sana na tunamshukuru sana. Pamoja na ukumbi huo, mahakama inajengwa pale Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko miradi ya Kitaifa ambayo inatugusa moja kwa moja, kama Bwawa la Kufua Umeme kule Mwalimu Nyerere. Bwawa lile linatoa umeme ambao unafika mpaka vijijini kwetu. Bila bwawa hilo, umeme usingewaka vijijini, na umeme wa *REA* ungekuwa hadhithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uko mradi wa reli ya *SGR* ambao tunatoka sasa Dodoma saa tatu, tutaenda Tabora kwa saa mbili au saa moja na nusu. Hii tuna imani kwamba, likishaisha mradi huu wa *SGR*, Tabora itanufaika ikiwemo Jimbo la Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia liko daraja la Kigongo Busisi ambalo limefunguliwa jana. Daraja lile ingawa lipo pembeni kwa kanda ya Ziwa, litaingiza fedha, lakini fedha zile zinakwenda *centralized* kule Benki Kuu na hiyo itatusaidia sisi kupata mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya mwaka huu, kwa sababu tunaiongelea, mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Kitila na Naibu Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni ya watu, na kama utaona huko mbele, kuhusu mpango wa kumalizia miradi ambayo ilikuwa imebakia mwaka 2024, na miradi ambayo ilitoka huko nyuma, tunampongeza sana Mama Samia kujiandaa pia kutoa ahadi alipoingia madarakani kwamba atamalizia miradi hii, watu hawakuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mama Samia, miradi moja moja inakamilika. Bwawa la Mwalimu Nyerere limekamilika, Daraja la Busisi limekamilika na reli ya kati inaenda vizuri. Tunampongeza sana kwa kutimiza ahadi hiyo. Ni utu kutimiza ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR,* Daraja la Busisi nimesema, lakini kwenye afya amefanya vizuri sana. Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi nzuri sana ya kujenga vituo vya afya, hospitali, pia vifaa vya tiba vimenunuliwa vingi. Tumeendelea kupata elimu bure, *REA* imeendelea na barabara zimeendelea kujengwa. Hizi zilikuwa ni ahadi za mwanzo za Mama Samia Suluhu Hassan ambazo amezitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuwasahau watu hawa ambao nimewataja; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Kitila, bajeti hii ni nzuri. Ngoja niyaseme yale ambayo yametugusa Wanauyui moja kwa moja. Amesamehe kodi ya ongezeko la thamani, viuatilifu vya dawa za mashambani za wakulima, pongezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesamehe pia *VAT* kwa ununuzi wa bima, amesamehe pia *VAT* kwa mafuta yanayotengenezwa hapa nchini, amesamehe *VAT* kwenye lami ili tujenge barabara, amesamehe *VAT,* magazeti sasa hawatakuwa wanazunguka meza kusomea magazeti mezani, watakuwa wananunua kwa sababu yamepungua bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Rais amesamehe *VAT* kwenye matanki ya mitungi ya gesi tunayopikia majumbani. Mimi nimekuwa mpenzi wa wazo la Mheshimiwa Rais la kupeleka nishati safi, nimekuwa nagawa mitungi ya gesi bure katika Jimbo langu na majiko; na kwa kupunguza bei, nitayagawa mengi zaidi. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mama Samia Suluhu Hassan, kwani jambo la kupeleka nishati vijijini lilikuwa na kasoro kubwa sana kwetu. Watu wanakuwa na macho mekundu wanaambiwa wachawi, halafu wanauawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imegusa mpaka bodaboda, imegusa mpaka bajaji. Hii ndiyo bajeti ya watu, bajeti ya wananchi, tunaita sisi bajeti ya wananzengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina salamu kwa wananchi wa Uyui waendelee kuniamini, tuliyoyafanya mengi sana wameyaona, lakini yako mengi ambayo tumeyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu mikataba ya wakandarasi. Tuna mikataba ya wakandarasi wa hapa nchini wazawa na mikataba ya wakandarasi wa nje.

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu unisikilize. Sisi wakandarasi wa ndani tukifanya kazi kama wakandarasi, tusipolipwa tunangojea mwaka, miaka miwili mpaka mali zetu tulizoweka benki zinachukuliwa. Tukilipwa hatutakiwi kuongeza riba yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi mzawa akiweka riba yoyote kwenye mkataba wake, anakuwa *black listed,* hapati tena kazi, lakini wenzetu wakandarasi wa nje wakichelewesha malipo yao, wanawekewa riba, wanalipwa na riba. Kwa nini tusifanye mikataba iwe sawa kunyanyua wazawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana. Kama kweli wewe ni mzalendo, ni ndugu yangu, na unatupenda sisi ndugu zako wazawa, tusaidieni wakandarasi wa Tanzania tuweze kulipwa kwa wakati unaofaa, pia kama tutacheleweshewa malipo na sisi tulipwe hata kidogo kupunguza gharama ya mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko pia suala la kupata mapato mengi kutoka kwenye makampuni ya ulinzi. Makampuni ya ulinzi binafsi hapa nchini hayana sheria na hayana kanuni. Matokeo yake hayajulikani mapato yake. Ningeshauri sheria ile ya sekta ya ulinzi binafsi, iletwe Bungeni hapa; niliiandika mimi kama Muswada binafsi, lakini ulichukuliwa na Serikali kwamba utaletwa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Hiyo sheria haijaletwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ile itatusaidia kupata mapato, kwa sababu makampuni yanajulikana. Pia kutakuwa na mamlaka ya kuongoza makampuni haya. Sasa hivi hayapati kazi kwenye Kimataifa kwa sababu hayana *classification*. Mamlaka hii ya sekta binafsi ya ulinzi itayapanga makampuni haya kwa mpango wa madaraja, na italeta faida nyingi kupata mapato ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana kwa muda wako, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Athuman Almas Maige kwa mchango wako.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia leo Bajeti Kuu ya Serikali. Awali ya yote, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa maeneo makubwa mawili. Kwanza, kunijalia afya na uzima katika kipindi cha miaka mitano nikiwatumikia akina mama wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru Mungu kwa kuijalia Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mafanikio makubwa ndani ya miaka mitan,o jambo ambalo kwa kweli linatupa ufahari na tunakwenda kwenye uchaguzi tukiwa na amani na tutatembea kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa aliyoyafanya katika Mkoa wa Tanga. Kusema kweli ni katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mikopo ya akina mama, huduma za

jamii, huduma za maji, huduma za afya, huduma za elimu zimeboreka na zimetoka kwa kiwango ambacho kwa kweli Watanzania wanaoishi katika Mkoa wa Tanga ni mashahidi mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza sana Waziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amekuwa Waziri wa Fedha kwa miaka mitano mfululizo. Hili jambo siyo jambo dogo, ameaminika, amefanya kazi nzuri. Mama yetu ameona ameweza kumsadia na ndio maana hakumhamisha, hakumwondoa, amempa Wizara ya Fedha kwa miaka mitano mfululizo. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hongera sana, Mwenyezi Mungu akubariki zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Msaidizi wake Mheshimiwa Chande, Naibu Waziri, kwa kweli ni watu waunguana sana. Naibu Waziri ni msikivu, anatusikiliza sana humu ndani, anatusaidia mambo mengi. Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya kazi nzuri ya kuunganisha watu wawili kuwaweka katika Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango na Naibu wake Mheshimiwa Nyongo. Hawa wawili walikuwa wenyeviti wangu wa Kamati wakati naingia humu Bungeni, na Mheshimiwa Mkumboameniachia Uenyekiti wa Kamati baada ya yeye kuteuliwa kuwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni watu ambao nawafahamu uwezo wao, ukarimu wao, weledi wao, wamekuwa ni washauri wakubwa hata baada ya wao kuwa Mawaziri, bado wameendelea kuishauri Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuendelea kufanya vizuri. Nawashukuru na ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitimisha Bunge la Kumi na Mbili na inawezekana mchango wangu ukawa ni mchango wa kuhitimisha Bunge kwa upande wangu. Nitumie fursa hii kwanza

kuwashukuru sana akinamama wa Mkoa wa Tanga. Walifanya maamuzi sahihi kunileta mimi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefanya kazi nzuri kwa ushirikiano na mimi kutekeleza mambo mbalimbali katika Mkoa wetu. Tumeshirikiana nao, tumefanya mambo mengi, tumefanya shughuli nyingi na hivi karibuni nimepita huko kwa ajili ya kufanya ziara katika wilaya zote tisa za Mkoa wa Tanga. Wakinamama wamenifanyia maombi, dua, na matambiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ishara kwamba bado wanatamani kuendelea kuwa na mimi binti yao Husna Juma Sekiboko kwenye Mkoa wa Tanga. Ninawashukuru na ninawaomba waendelee kuwa na moyo huohuo. Mitano ijayo tutafanya mambo kwa *5G* kama ambavyo tumekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo sasa nijikite kwenye Bajeti ya Serikali. Kwanza nianzie na pongezi kwenye Bajeti ya Serikali ambayo nimeisoma; 18% ya Bajeti ya Serikali imekwenda kwenye Sekta ya Elimu. Hii ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inanyanyua viwango vya elimu nchini. Pia, inatoa fursa kwa Watanzania wengi zaidi kuweza kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme kwamba bajeti ya kimataifa kwa viwango vya kimataifa tunatakiwa kila mwaka Serikali itenge 20% ya bajeti yake kuu ya Serikali kwenda kwenda kwenye elimu. Sisi tupo kwenye 18%; ni asilimia nzuri, kubwa na tunadhamiria kwenda kwenye viwango vya kimataifa. Tukiendelea kuongeza Bajeti ya Elimu kuanzia Elimu ya Msingi, Elimu Sekondari mpaka Elimu ya Vyuo Vikuu maana yake kwa miaka michache ijayo Tanzania itakuwa imefanya mapinduzi makubwa sana ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaakisi maboresho ya elimu yanayofanyika kwenye elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Tumefanya mabadiliko makubwa kwenye mitaala na Sera yetu

ya Elimu. Kwa kweli kwa miaka michache ijayo tutaanza kunufaika na mabadilko haya. Binafsi sina hofu na wasiwasi na utekelezaji wa mitaala mipya. Ninaamini kwamba fedha zikiendelea kutoka kama ambavyo bajeti imepangwa vizuri, basi nchi yetu itaendelea kunufaika katika eneo hilo na hakika tutakwenda kwenye viwango vya elimu vile ambavyo tunavitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu dogo ambalo leo nilitamani kulitolea ushauri ni Elimu ya Juu (Elimu ya Vyuo Vikuu). Tumejenga vyuo vingi vizuri Tanzania vya binafsi na vya umma lakini tuna changamoto kubwa kwenye vyuo vyetu. Changamoto yenyewe ni kuhusiana na mitaala yetu ya elimu ya juu. Bado tunazalisha wanafunzi vyuo vingi kwa kutamani kupata ada kwa maana ya kutafuta fedha kufanya biashara, lakini bado hatujajikita katika kuzalisha wanafunzi au wahitimu kulingana na uhitaji wa changamoto zilizopo kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme ili twende na elimu ambayo inakwenda kunufaisha umma wa Watanzania, ili kupunguza ombwe hili la watoto wengi kuhitimu vyuo vikuu na kukosa ajira, ni lazima vyuo vyetu vya *public* na *private* viamue kulichukua suala la ajira kuwa ni jukumu la vyuo kuhakikisha kwamba kila chuo kinapozalisha watoto kinahakikisha kimewaandalia soko, kimewa-*connect,* kimewaunganisha na viwanda, taasisi na masoko ya ajira. Hili litatusaidia kupunguza ombwe kubwa la kukosa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea nchi kama Morocco. Morocco wanafunzi wao wanaozalishwa kwenye vyuo, kila chuo kimekuwa *tasked* kwamba 60% ya watoto wanaohitimu kwenye chuo hiko lazima waunganishwe na masoko ya ajira moja kwa moja. Wao wametoka nje ya boksi wanawaunganisha na masoko Ujerumani, Uingereza na Ufaransa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi kabla hajahitimu shahada yake tayari ameshaunganishwa wapi anakwenda kufanya kazi. Sisi hili Tanzania bado hatulifanyi kwa sababu vyuo vyetu vimejikita katika kutafuta ada zaidi. Utakuta hata kozi

zinazotolewa sehemu kubwa wanafundisha *sociology* na *education* ambayo pengine hata kwenye kuajiri wapo walimu wengi mtaani bado hawajapata ajira. Wanafundisha kozi ambazo ni rahisi kupata wanafunzi ili waendelee kukusanya ada, lakini wanasahau kuwaunganisha hawa wanafunzi na masoko ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu; mitaala yetu ya Vyuo Vikuu inavyoandaliwa taasisi zinazoajiri zishirikishwe, ili ziweze kutoa *qualities* (vile vitu ambavyo wanavihitaji kwa mhitimu) ili mhitimu anavyomaliza masomo awe moja kwa moja anakwenda kwenye eneo ambalo anategemewa kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ufundishaji na utoaji wa kozi hizo ni vizuri vilevile kuwashirikisha waajiri, wahitimu wetu wakiunganishwa moja kwa moja wakati wa masomo na baada ya masomo na masoko ya ajira maana yake tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa ombwe hili la ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu lazima iwe ya kimataifa. Ni lazima tu-*internationalize* elimu yetu. Tukiweka elimu ya kimataifa maana yake hatutapambania tu nafasi za ajira zilizopo nchini bali tutaendelea kunufaika na nafasi za ajira ambazo zipo nje ya mipaka yetu. Leo tumeona *VETA* wameanza, wanaanza kuzalisha wachimbaji wa madini wanakwenda nje ya nchi. Sasa, tukienda kwenye vyuo vyote vya *private* na *public* (umma na binafsi) wakazalisha watoto kwa njia hiyo, maana yake mwisho wa siku baada ya miaka kadhaa pengine nchi yetu sasa tutakuwa tunaimba wimbo tofauti wa ukosefu wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwenye simu za Waheshimiwa Wabunge hapa kila mzazi analalamika mtoto wake aajiriwe, lakini chuo kimemzalisha na hakihusiki. Baada ya mtoto kuhitimu chuo kimenawa mikono hakihusiki na huyo mtoto anakwenda wapi? Sasa ni lazima hivi vyuo viunganishwe vipewe jukumu la kuhakiksha kwamba, wahitimu wao wana-*quality* ya kuliwa na soko gani? Baada ya watoto kuhitimu wanakwenda kumezwa kwenye soko lipi la ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia kuondoa kozi zile ambazo hazina ajira lakini vyuo viweze kuzalisha kozi ambazo zinaandaa wanafunzi moja kwa moja kwenda kwenye soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema hivi. Wakati tunaingia hapa 2021, moja ya kelele ambazo mimi binafsi nimepiga sana ni kuhakikisha kwamba Serikali inafanya mabadiliko katika mitaala ya elimu iweze kuajiri na watoto waweze kujiajiri. Leo tumeshapata mitaala mipya (nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan) ambayo watoto wanakuja na kozi tofauti kulingana na vipaji vyao kuanzia Shule ya Msingi mpaka Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti zetu huko mbele tunapokwenda lazima tujikite sasa kwa hawa ambao wamekuja na elimu ya ufundi, amali, *music,* michezo na kadhalika; baada ya kuhitimu elimu ya sekondari maandalizi ya wao kwenda elimu ya juu yakoje? Ni vyuo vyetu hivi sasa vianze kujibadilisha mapema kabla hatujatengeneza huo msongamano wa wanafunzi ambao wamehitimu wakakosa nafasi ya kwenda kusoma kwenye elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nikushukuru sana wewe binafsi, niushukuru Uongozi wa Bunge, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Serikali nzima pamoja na Mawaziri wote kwa ushirikiano ambao tumepata katika Bunge hili kwa miaka mitano. Tunaomba Mwenyezi Mungu kwa kweli atusaidie turejee tuendelee kufanya kazi hii ya wananchi na Tanzania ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa njema na kuwa Taifa lenye ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na uongozi wote wa Bunge. Mwenyezi Mungu awabariki sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Nilimwita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Kavejuru Felix atafuata na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile atafuatia baada ya hapo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii adhimu na adimu ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya mwisho katika kipindi chetu cha kuhudumu katika Bunge hili. Ninamshukuru Mungu kwa neema ya uzima aliyonijaalia mpaka leo nipo imara na nipo tayari kwa mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nianze kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kweli amesimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na nchi yetu imeendelea kupaa kimaendeleo katika ramani ya dunia. Rais Dkt. Samia kwa kweli anastahili maua yote. Hakuna wa kumfikia; kwa hiyo, mitano tena inamstahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza vilevile Makamu wa Rais Dkt. Mpango kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake. Nikiendelea ninampongeza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, Naibu Waziri Mkuu Dkt. Doto Biteko. Ninawapongeza sana Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyofanya kazi iliyotukuka ya kuisaidia Wizara ya Fedha ikaweka katika medali hii iliyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba nimpongeze sana Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Rais wa Mabunge ya Dunia kwa jinsi alivyotuendesha katika majukumu yetu kwa miaka mitano yote iliyopita kwa umahiri na uhodari wa pekee. Mheshimiwa Dkt. Tulia anaweza na anaweza kabisa. Niwaombe tu wananchi wa Uyole waitunze tunu hii na kuipatia stahiki yake inapofika mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Naibu Spika *Comrade* Zungu na yeye kwa jinsi alivyosaidiana na Spika. Ninawapongeza Wenyeviti wote; wamefanya kazi nzuri sana iliyotukuka kutuongoza sisi katika Bunge hili kipindi chote tumekuwa na nyie. Ninawashukuru na kuwapongeza Wabunge wenzangu wote kwa jinsi tulivyoshirikiana na *insha Allah* kwa uwezo wa Mungu, sote tutarudi tena hapa kwa kasi kubwa zaidi tuendeleze yale ambayo yalikuwa labda yamebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kutoa shukrani pia kwa watu wangu wa Mkoa wa Mjini ambao kwa mamlaka yao waliyokuwa nayo ndiyo wamenileta hapa kuwa Mbunge wa Mkoa wa Mjini, kwa maarufu wananiita Asha Mshua. Nimekuja hapa kutumika, wenyewe wameniona nikiwa na magongo matatu, gongo moja, lakini sikurudi nyuma, uongo kweli? Kwa hivyo, watu wangu ninasema ahsanteni sana na ninaamini watanipatia tena nafasi hiyo ya kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hii bajeti kusema kweli bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeonesha dira ya kujinasua kiuchumi na kuelekea kwenye kujitegemea asilimia kama nchi. Pamoja na kuwa ni bajeti ya maono pia imeonesha dhamira ya dhati kupunguza utegemezi wa misaada ya kigeni. Pia, imetoa nafasi kwa matumizi ya kilimo hai, kuelekeza ukombozi katika uagiziaji wa mbolea, kemikali na viuatilifu sumu kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo shida kutengeneza viuatilifu salama; ni kujiamini na kulifanya kazi suala hili. Kilimo chetu ambacho ndio uti wa mgongo kinakwenda kupaa, ili mradi tukiongeza nguvu katika kuhimiza kilimo cha *style* hii ya kilimo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti pia imegusia nchi kutengeneza wenyewe dawa au kununua kwa mapato yetu ya ndani. Watanzania tuwatibie wagonjwa wetu badala ya kusubiri. Kwa mara ya kwanza Serikali imeondosha utegemezi kwa misaada ya kigeni. Mfano, Serikali kujitolea kununua dawa za *ARV*

ni jambo la ukombozi mkubwa sana na limeonesha ukomavu wa Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imejikita sana katika kukamilisha miradi elekezi na kuimarisha rasilimali yetu katika sekta za kijamii. Mfano, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo. Jambo zuri kabisa na la muhimu nikwambie Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni hili la kuahidi hapa Bungeni kwamba Uchaguzi Mkuu unakwenda kugharamiwa na sisi wenyewe kwa fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia katika hatua hizi juzi Daraja la Kigongo – Busisi (Daraja la JPM), limezinduliwa na mwenyewe Mama Samia. Huu ni ukombozi mkubwa sana wa miradi mikubwa kama hii ambayo tunaahidi tunakwenda kuimalizia. Hii inasaidia kufanya urahisi katika maeneo yale na kwa hivyo kunyanyua kuichumi na kuwaondolea kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine zuri sana ambalo Wizara ya Fedha wamefanya ni kule kuchambua na kuimarisha *relation* baina ya *TRA* na wafanyabiashara na kuwaondolea ile bughudha ya kukamatwa au kufukuzwa ila kuwaongezea elimu ambayo inawapelekea wao watalipa kodi kwa hiyari. Kwa hivyo, kodi nyingi itakwenda kupatikana na ni wajibu kulipa kodi kwa sababu kodi ndio misngi wa maendeleo. Hao wote tunawaona wameendelea, wanalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa ninavyofahamu mimi, kule ukikwepa kodi adhabu yake inakuwa kubwa unaweza hata ukafungwa. Kwa hivyo, hapa *TRA* na wenzetu watachukua lugha laini watubembeleze mpaka tufahamu umuhimu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo linaikumba hii Wizara ya Fedha. Ninataka ni-*quote* agizo fulani hapa kwamba, “wapo watu wanadai fedha kwa miaka mingi na hawalipwi mpaka wengine wamekufa”. Ninashukuru kwamba tatizo hilo lilikuwepo kwa wateja wa *FBME* lakini wameanza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia wafanyakazi wanadai haki zao za msingi kutoka kwa Mwajiri *TTCL*. Wafanyakazi 283 tangu 2018 ambapo wafanyakazi hawa kiongozi wao ni Fidelis Msamila na wenzake hao 283. Hawa watu baadhi yao wengine hata wameshafariki na ni-*quote reference* ya madai yao; "*CMA/BSM/ILA/R.592/2023*". Hawa watu wanadai fedha zao; hebu Mheshimiwa Waziri akaangalie. Bajeti yetu nzuri namna hii kwa nini watu wengine waendelee kuteseka? Hebu kafanye uchunguzi hawa watu walipwe, tusitie doa bajeti yetu ambayo ni nzuri kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi, sina cha kuongeza sana. Ninaridhika na *speed* inayokwenda na kwa maana hiyo ninasema kwamba kwa kweli mitano tena ndio inamstahili Mama Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote. Kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amefanya kazi nzuri ya kuhudumu bila kutetereshwa kipindi chote kile; wewe *my boy you are really my son*. *I admire and appreciate you, and I love you. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba kuna maboresho katika mifumo ya kodi na ku-*harmonize* mifumo ya kodi. Tumeona hilo ni jambo linakwenda kusaidia kwa hiyo kutakuwa hakuna ubabaishaji. Kwa hivyo, niseme kwamba kwa kweli kwa hakika hasa hii bajeti yetu imetengenezeka vizuri sana. Niombe tu kwamba tuendelee kuunga mkono Serikali yetu, yale ambayo hayajakamilika tuweze kuyamaliza na tukumbushane wajibu wa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema ahsanteni sana. Wote wamenipenda sana, wameniuguza sana, mpaka wakanipa ile *tittle* kwamba, mimi *Miss* Bunge. Ninasema ahsanteni sana, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, maarufu kwa jina la Mshua.

Nilimwita Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii ambayo umenipatia. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na nchi kwa zawadi ya uhai. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutubariki sisi sote kuwepo mpaka kwenye hii bajeti ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi ya pekee kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya pamoja na Makamu wake wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa shughuli kubwa kwa ujenzi wa Taifa letu na Taifa letu linasonga mbele. Pili, ninawashukuru na ninawapongeza Mawaziri; Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Mwalimu Chande, kwa mafanikio na miradi mikubwa ambayo tunaona wamekuwa wakiitolea fedha na imetekelezwa majimboni. Wenye macho wote wameona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Mkumbo, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Nyongo. Hakika kwenye bajeti hii, kwenye Wizara hii, tumeona mipango mingi ambayo mmeiweka, kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mungu na ninawashukuru Wanabuhigwe, nimekuwa nao takribani kwa miaka mitano sasa. Tunajua wilaya yetu ilivyokuwa, katika uongozi huu wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaidiwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, ambaye ni Mwanabuhigwe, tumeona Buhigwe inayokimbia kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huduma za afya tumejengewa hospitali ya wilaya, imekamilika, ina vifaatiba, ina wataalam na tayari inatoa huduma. Tumepata vituo vya afya vinne; vitatu vimekwishakamilika na cha nne kinaendelea kujengwa. Serikali imetujengea zahanati zaidi ya 10 na shughuli bado inaendelea. Tunasema ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Buhigwe Oktoba tunatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye afya; kwenye elimu tumeona shule mpya zimejengwa, shule za msingi na za sekondari. Kwenye bajeti hii nimeona kuna ujenzi wa Chuo cha TEHAMA ambacho kinaenda kujengwa katika Wilaya ya Buhigwe kwenye Kijiji cha Songambele. Buhigwe ikifika Oktoba tunatiki, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka kwenye elimu; kwenye barabara tumeshuhudia, kupitia *TARURA,* tumechonga na kuimarisha barabara nyingi, vijiji vyetu sasa vinafikika na wakulima wanasafirisha mazao yao ya kilimo pasipo na shaka. Hongera sana Waziri wa Fedha, hongera sana Waziri wa Mipango, kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye huduma ya maji. Tuna vijiji 44 ambavyo hakuna hata kimoja ambacho kakijapata maji. Vyote vina miradi inayoendelea na mingine imekamilika. Tunasema ahsante sana. Wanabuhigwe ikifika Oktoba wako tayari kutiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwa wakulima. Tumeshuhudia pembejeo ambazo zimemwagika kwenye kilimo, tumepata mbolea ambayo tumekuwa tukiinunua ikiwa tayari Serikali imekwishalipia nusu ya gharama. Wakulima wa kahawa wamefaidika, wakulima wa tangawizi wamefaidika, wakulima wa mahindi wamefaidika, kila mkulima amefaidika. Kwa nini tusitiki? Oktoba tunatiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye miradi ambayo sasa imeufungua Mkoa wetu wa Kigoma. Tumekuwa tukilalamika juu ya mkoa wetu kuunganishwa na mikoa mingine, tukitoka

Kaskazini ya mkoa wetu kuelekea Mwanza tumepata barabara, ambayo imejengwa, Barabara ya kilometa 268 kutoka Kabingo katika Wilaya ya Kakonko, ya Mheshimiwa Kamamba ambaye ninaamini naye watamrudisha, imekuja Kibondo, imekuja Malagarasi, imekuja Kasulu, imekuja Manyovu. Nayo sasa imekamilika, wilaya zote hizo tunaenda kutiki mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kutuunganisha na Tabora, tulikuwa tumebaki na kilometa 51 kutoka Malagarasi mpaka Uvinza. Sasahivi mkandarasi yuko pale, zimebaki tu kama kilometa 17, na hazifiki na kazi iko inaendelea. Sasa mkoa wetu umefunguka unaenda kuwa korido ya biashara, tunaenda kufanya biashara sasa na Burundi, Kongo, Zambia na nchi zote zinazopakana na sisi. Kigoma Oktoba tunatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi tumeona ujenzi wa *SGR* ambao umeanza kutoka Tabora kwenda Kigoma, kilometa 506. Kama hiyo haitoshi kuna ujenzi wa reli ya kisasa, *SGR,* inayotoka Uvinza kwenda Msongati, kilometa 282. Wakandarasi wako *site* na reli hii inapita mpaka Jimbo la Buhigwe kwenye Kata ya Kajana na Kilelema. Kigoma mwezi Oktoba tunatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tunaona Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Kigoma mkandarasi yuko pale, majengo yako yanaota kama uyoga, uwanja unapanuliwa sambamba na mji ambao sasa uko chini ya Mheshimiwa Ng'enda Kilumbe. Lami iko inajengwa kila kona, ninaamini na Kigoma Mjini watatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna ujenzi wa kiwanda cha meli na ukarabati wa meli. Kwenye bajeti hii tumeona fedha zinaenda kutolewa na tayari ukarabati wa meli umekwishaanza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Wapi Taarifa?

Aah Mheshimiwa Jumanne Mtaturu.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajaribu kumpa Taarifa mchangiaji anayechangia vizuri, ndugu yangu Mheshimiwa Kavejuru kwamba, ukipewa mtihani ukafanya vizuri na ukapata matokeo lazima upate tiki. Kwa hiyo, ninakubaliana na yeye kwamba, tunatiki Oktoba itakapofika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru, unaipokea Taarifa hiyo toka kwa Mheshimiwa Mtaturu?

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea hiyo Taarifa ya kaka yangu Mheshimiwa Mtaturu kwa mikono yote miwili. Mungu akubariki sana na wewe huko kwako wanatiki na wewe unarudi, Novemba tuko wote hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, upo ujenzi wa kiwanda cha meli. Zipo meli mbili, nne pale ziko zinajengwa, lakini ukarabati wa meli ambazo ni pendwa, *MV Liemba na MV Mwongozo,* tayari umeanza. Kwa hiyo, sasa wananchi wanaokaa kandokando ya Ziwa Tanganyika katika Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na nchi jirani tukichukua Zambia, tuje na upande wa Kongo, Moba, Kalemie, Ubwari na Bujumbura, Kigoma wanaenda ku-*enjoy*. Muda si mrefu tutaenda kuongeza mapato na kuchechemua uchumi wa Kigoma kwa kupitia biashara kwa hiyo, Mwezi Oktaba, Kigoma inatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa sababu kwa nini Kigoma tunaenda kutiki, kama shukrani yetu kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wake wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, ninarudi kwa wananchi wa Buhigwe. Ndugu zangu wananchi wa Buhigwe nimekuwa pamoja nanyi kwa unyenyekevu, tumefanya kazi wote kwa pamoja, wanaosafiri huwa wanaanza safari pamoja. Niko na nyie, tumelala pamoja, tumefanya kazi kwa pamoja, na wanaotafuta kuni ndiyo wanaoota moto pamoja. Ndugu zangu wakati umefika tena,

wanasema chanda chema huwa kinatunzwa; anayefanya kitu kizuri huongezwa. Ninaomba waniongeze miaka mitano tena, nitaendelea kuwa mwaminifu mbele yao na mbele ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninawashukuru viongozi wa ngazi ya wilaya, Mheshimiwa Kanali Michael Masala Justin Ngayalina, Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Kamati ya Ulinzi na Mkurugenzi Mbilinyi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kusimamia miradi ambayo imeletwa na Serikali. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kigoma na Buhigwe Oktoba tunatiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Kavejuru.

Namuita sasa Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo atafuata na Mheshimiwa Atupele Fredy ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti iliyoletwa na Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji. Mimi naungana na Wabunge wenzangu kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi na uhai, ametulinda sasa tunapokwenda kukamilisha miaka mitano. Kipekee ninamshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaungana na Wabunge wenzangu kumshukuru sana kwa namna ambavyo ametuletea miradi mingi katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Tamisemi kwa kipindi chote cha miaka mitano kwa hiyo, nimezunguka sana kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo. Ukiangalia miradi mikubwa inayotekelezwa kwenye kila kona ya nchi yetu hakuna ubishi Mheshimiwa Rais anakwenda kupata kura za kishindo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote. Wameendelea kunipa ushirikiano, kama Mbunge wa Jimbo la Nachingwea na kuhakikisha kwamba Nachingwea inaendelea kupiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia, viongozi wangu wa chama, Wilaya ya Nachingwea na wana-CCM wenzangu wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mwalimu Longinus Nambole kwa namna walivyonipa ushirikiano. Ninawashukuru pia, wapigakura wote wa Jimbo la Nachingwea. Ninaendelea kuwashukuru viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Lindi wakiongozwa na Alhaji Hassan Jarufu, Mwenyekiti wetu bingwa, kwa namna walivyonipa ushirikiano, wakanifundisha na kunielekeza kuhakikisha kwamba, ninatimiza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuishukuru familia yangu iliyonivumilia nyakati zote wakati ninatimiza majukumu yangu, ikiongozwa na mke wangu kipenzi Eva Bipaulo Komu. Wamefanya kazi kubwa ya kunivumilia, lakini pia, kuniombea na kuhakikisha kwamba, ninatimiza majukumu yangu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kujielekeza kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni ya viwango, ni bajeti ambayo inaendelea kujibu shida na matatizo ya nchi yetu. Ninaendelea kuunga mkono hoja hii maana unaweza ukahutubia sana halafu ukashindwa kuunga mkono hoja. Ninaunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ambavyo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anavyoitendea haki Wizara hii na tukienda kwa Mheshimiwa Profesa Mkumbo kwa namna ambavyo anaendelea kuweka mipango sawasawa kuhakikisha nchi yetu inakimbia kimaendeleo, pamoja na Manaibu wao na wataalam wote. Ni wazi kwamba, jambo hili ni kwa sababu ya kiutaratibu tu, lakini ilikuwa tayari tuwe tumeshamaliza na bajeti hii tumepitisha, ili kazi kubwa ambayo iko kwenye mipango iende

ikatekelezwe. Tukisema Mheshimiwa Rais mitano tena, tunamaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba, nimezunguka maeneo mbalimbali nikiwa na Kamati ya TAMISEMI kukagua miradi ya maendeleo, sasa hapa nitajielekeza kidogo kwenye Jimbo langu la Nachingwea. Mwaka 2020, 2021 na 2025 tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 101 katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Kiasi hiki cha fedha hakijawahi kupatikana kwa kipindi kama hiki tangu enzi za uhuru. Ninarudia tena, kiwango hiki cha shilingi bilioni 101 hakijawahi kupatikana kwenye Jimbo langu la Nachingwea kwa kipindi kama hiki tangia uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili sasa, tunamwambia Mheshimiwa Rais hana tatizo kule Nachingwea na sisi hatuna deni na yeye. Tumekubaliana na hii nasema kwa ujasiri, wananchi nimewatembelea nimewaaga ninakuja hapa kwenye Bunge la Bajeti na wakaniambia kaseme, sisi 2025 tunakwenda na Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatolea mfano tu kwenye eneo la elimu, hapa tumepata shilingi bilioni 5.9 tumejenga shule mpya za sekondari tano, za kisasa, nzuri kabisa. Hizi shule tulizoea kuona aidha vyuo au za misheni ambazo zilikuwa nzuri, leo tunashuhudia ni shule za sekondari ambazo zinamilikiwa na Serikali, nzuri, zikiwa kwenye viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tumepata shule mpya za kisasa za msingi tatu, hizi shule ni za mfano. Kwenye ziara yangu nilikwenda sehemu moja nikamkuta mama akanitolea ushahidi, saa tisa usiku mtoto anatamani kwenda shule, saa tisa usiku. Ni kwa nini anatamani kwenda shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yaliyowekwa yanamfanya mtoto huyu apende kusoma. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la elimu bila ada, tumepokea zaidi ya shilingi bilioni saba. Hili ni jambo kubwa na

hapa sasa imeendelea kutoa morali kwa wanafunzi na walimu kwa sababu, inajumuisha pia, fedha ya madaraka. Walimu wa Nachingwea sasa wana morali ya kufundisha na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Shule ya *VETA* yenye thamani ya 1,400,000,000. Haya mambo tulikuwa tunayaona tu maeneo mengine, lakini leo shule hii mpya ya kisasa ya ufundi inajengwa na kazi hiyo inaendelea kwenye jimbo langu la Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la afya tumepokea zaidi ya shilingi bilioni saba, eneo hili nitakwenda polepole kidogo. Wakati tunaingia mwaka wa fedha 2020/2021 tulikuwa na kituo cha afya kimoja, hiki ndicho kilikuwa kinafanya kazi na kulikuwa na kituo kingine cha pili ambacho kimsingi ilikuwa ni zahanati, lakini ilipewa hadhi ya kituo cha afya. Sasa ninapozungumza tunavyo vituo vya afya vizuri na bora, ambavyo vinatoa huduma zote sita. Maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia uhuru mpaka Mwaka wa Fedha 2020/2021 tulikuwa na kituo cha afya kimoja ambacho kilikuwa kinafanya kazi. Ongezeko la vituo vya afya vitano katika miaka minne na nusu, miaka mitano, hili ni jambo kubwa. Viko vituo vya afya vingine ambavyo vinaendelea na ujenzi na viko kwenye hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la barabara, tumepokea zaidi ya shilingi bilioni saba. Kazi hiyo inaendelea, lakini hii haijumlishi barabara zingine ambazo zinaendelea kutekelezwa; kwa mfano ujenzi wa Barabara ya kutoka Ruangwa kuelekea Nachingwea kwa kiwango cha lami, mkandarasi yuko *site* na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la maji tumepokea zaidi ya 4,700,000,000 na hii haijumlishi Mradi mkubwa wa Maji kutoka Nyangao kwenda Nachingwea, ambao pia, unapeleka kwenda kulisha kwenye Jimbo la Ruangwa, zaidi ya shilingi bilioni 100. Hili ni jambo kubwa na huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, ambaye tunasema mwaka huu tunakwenda kumlipa wema kwa kumpa kura nyingi za ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeona Wabunge wenzangu wananiambia kwamba, kwao wataongoza kumpa kura za heshima, za ndiyo, Mheshimiwa Rais. Kule Nachingwea tumekubaliana tutampa kura nyingi za kishindo na tutaongoza kwenye majimbo yote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la nishati. Wakati tunaingia mwaka wa fedha 2020/2021 vijiji 57 ndiyo vilikuwa na umeme na Nachingwea ina vijiji 127, vijiji 70 vilikuwa havina umeme. Sasa hivi ninavyozungumza vijiji vyote 127 vina umeme muda wote na kazi za wananchi za kujiletea maendeleo zinaendelea. Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo nako Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana na upo wimbo kule wenzetu tunaimba; ni kanuni tu vile haziruhusu, ningeunganisha hapo ungeuona huo wimbo ambao unamsifia Mheshimiwa Rais. Korosho ndiyo dhahabu ya Kusini. Rais amefanya uwekezaji mkubwa kwenye eneo hili na ametupa pembejeo bure kwa miaka minne yote mfululizo; hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa pia niende kidogo na Mheshimiwa dada yangu Dkt. Thea Ntara, alikuwa anasema kule Lindi sasa nyumba; nafikiri yeye alipita miaka ya zamani; nyumba zilizopo kule si dhaifu tena, kule wananchi sasa wamechangamka na maendeleo yanakwenda. Tunachokubaliana hapa ni kwamba maendeleo ni hatua. Wapo wengine bado wanaendelea, lakini watu wengine wamekwenda mbele sana. Kwa hiyo kazi kule inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pia zaidi ya shilingi bilioni tatu na milioni 700 kwa ajili ya kujenga jengo la utawala, kazi hiyo inaendelea. Huyo ndiye Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo yule ambaye anasema kwamba tunakwenda na uchawa tu wa kusema mama Samia mitano tena; mama Samia amefanya. Ametekeleza na mengine ambayo hayakuahidiwa katika Ilani ya

Chama Cha Mapinduzi. Ukiingia leo kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, hospitali kongwe imefanyiwa ukarabati mkubwa, tumetumia zaidi ya shilingi milioni 900. Unakwenda majengo yameota, mapya, *ICU* mpya na ya kisasa; ndizo *ICU* zinazotumika ndugu zangu huko duniani, leo *ICU* ile ipo Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujajenga *ICU* ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanapata maradhi ya kwenda *ICU*, tunajenga *ICU* ili kuwa na utayari pindi yanapotokea maradhi ambayo yanahitaji mgonjwa kuwa na uangalizi maalum, tunampeleka kwenye hiki chumba. Huyo ndiye Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu; kwa wale waliotoka zamani Nachingwea leo wakiingia asifike usiku, vinginevyo basi awe na namba ya ndugu yake ili kuhakikisha kwamba anapata mawasiliano. Akifika mji unapendeza kwa mataa na barabara za lami zinaendelea. Kwa hiyo asije akashangaa shangaa akajikuta anapita wakati hapo ndio kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaona umewasha *microphone;* wananchi wa Jimbo la Nachingwea, hawa ni watu wema sana, wamenipa ushirikiano kutimiza majukumu yangu ya Kibunge. Wapo wengine ambao wananiambia Mheshimiwa Mbunge, bado tunakuona una nguvu na ninawaambia Mwenyezi Mungu, akipenda wakati ukifika Chama changu Cha Mapinduzi kikinipa ridhaa nitarudi tena kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwatumikia wana Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chinguile, kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete atafuatia, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja mbili

zilizopo mezani. Kwanza nianze kuunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuiongoza nchi yetu vyema. Kwa kuwa Serikali ni ya Chama Cha Mapinduzi na yeye ndiye Mwenyekiti wetu; kwa kweli kwa namna ambavyo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa miaka hii minne imetekelezwa kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia kaka zangu Waheshimiwa Mawaziri wote; Mheshimiwa Kitila Mkumbo, kwa sababu yeye ndiye mkubwa, Mheshimiwa Mwigulu ni mdogo wake; lakini wote kwa kweli ni marafiki zangu, pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa kazi njema wanayoifanya katika nchi yetu. Nimekuwa nikisema, kwamba anayefanya kazi njema amekuwa akifanya ibada. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu ataendelea kuwalipa na awaongoze katika majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hizi zote mbili ninataka kusema kwamba imeonesha umahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miaka minne ambayo ameiongoza nchi yetu. Nikinukuu kitabu cha Waziri wa Fedha, katika ule ukurasa wa 20 yeye amesema kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imekuwa ikitekeleza, ikiendelea na ile vita vya wale maadui watatu; ujinga, umaskini na maradhi. Ninataka niseme kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na huu mchakato wa vita ulianza tangu kipindi hiko, lakini kipindi hiki hii vita imepigwa kwa kishindo kikubwa sana, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye eneo la ujinga kila Mbunge huku ndani amesema namna shule shikizi zilivyojengwa, shule za msingi, shule za sekondari pamoja na zile za chini na za *A level.* Vilevile vyuo vya kati, vyuo vya ufundi, *VETA*, vyuo vikuu na namna ambavyo mafanikio makubwa katika sekta ya elimu yamefanyika. Hapo ndipo tunasema kwamba kishindo kwenye hili eneo la huyu adui ujinga Dkt. Samia ametekeleza kwa kishindo kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umaskini, kama ambavyo tunaona, pamoja na mambo mengine yote, lakini ninaangalia lile eneo la Watanzania walio wengi, wakulima, kwa kupeleka ruzuku ya mbolea; na kule kwetu tumesema viuatilifu; kwa namna ambavyo uzalishaji umeongezeka na kuongeza fedha za kigeni kwenye yale mazao ya kimkakati. Unaona kabisa kwamba hayo matokeo yamewafikia wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la maradhi, ukiacha zahanati zilizojengwa kila Mbunge hapa amekuwa akisema, pamoja hospitali za wilaya za kisasa, kama alivyosema Mbunge aliyomaliza kusema sasa hivi. Tumeona Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kujenga hospitali katika kila halmashauri. Hapo sasa tunaona kwamba kwa kweli amepunguza vifo vya watoto wachanga na akinamama wajawazito wakati wa kujifungua; na kwa ajili hii anatambulika duniani. Kwa hiyo ndiyo maana tunasema kwamba kwa hawa maadui watatu, pamoja na kwamba ilianza wakati ule, lakini katika kipindi hiki hawa maadui wamepigwa kweli kweli. Kama ni Nduli Idi Amin haya maadui matatu yamepigwa kuliko ilivyokuwa Nduli Idi Amin. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze sasa kwenye hizi hotuba zote mbili. Nikianza na baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema, baadhi ya maeneo mahususi ya kipaumbele, ule ukurasa wa 71; yeye ametuambia kwamba moja wapo ni kuimarisha sekta za uzalishaji zenye matokeo chanya katika kukuza uchumi, katika kukuza uchumi. Hapa ninaomba nijielekeze kwenye mambo machache yafuatayo; hasa nikijielekeza katika Mkoa wa Mtwara. Ninaamini moja ya sekta ambayo imo na ambayo imewekewa kipaumbele ni miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba sana na niishauri sana Serikali yangu sikivu. Reli ya Kusini, niliuliza swali hapa kwamba je, Serikali inafahamu nguvu ya uwepo wa reli ya Kusini? ikajibu imeshafanya tathmini na inafahamu na kwamba ina matokeo chanya mengi na hasa katika kuzingatia kwamba tutaunganisha na Liganga na Mchuchuma; lakini na zile fedha zilizotolewa na Serikali kwenye bandari yetu ya Mtwara.

Mhesimiwa Mwenyekiti, ninatambua, kwamba kwenye Ilani yetu ambayo tayari imeshatolewa tutaitumia 25 – 30 hii reli ya Kusini imeandikwa mara kadhaa. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa mchakato ule wa Ilani, Profesa Kitila Mkumbo, kwamba hii ameitambua na hivyo Serikali imefanya tathmini na kuona matokeo ama matokeo chanya yatakayoletwa na reli ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu chake cha mpango ameandika kwa mistari miwili tu; kwamba Serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa reli ya Kusini katika hataua za awali zile kilometa 1,000. Ombi langu hapa ni kwamba, badala ya kuendelea na ule mchakato wa *PPP* ninaomba Serikali kwa yale mataokeo chanya yatakayotokana na reli ya Kusini Serikali ione haja ya kujenga yenyewe; huyu mwekezaji aje kushughulika na mambo mengine, ikiwemo *operations* kama itaonekana inafaa. Kwa sababu tukisubiri *PPP* hii itachukua karne nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili naomba sana, wakati anataka mipango ya nchi yetu iendelee kama ilivyo na ili tuendelee kupata fedha zingine ili Watanzania tuendelee kuneemeka katika sekta zote, hasa sekta za huduma ya jamii ambayo kwenye vipaumbele ipo, reli ya Kusini ni muhimu sana ikazingatiwa na kujengwa na Serikali katika mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninaomba katika hiyo hiyo miundombinu ni Mradi wa *LNG*. Ninataka niseme, wananchi wa Mtwara na Lindi wamekuwa na matumaini kwa muda mrefu. Sasa ninaomba haya matumaini kwa kipindi hiki yasiishie hewani. Ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan; yeye alifufua majadiliano yale ya mkataba na ninaamini yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba nishauri; ushauri wangu ni kwamba, ninaomba juhudi ziongezwe katika kutafuta gesi asilia na mafuta hasa Mtwara na Lindi. Siyo tu juhudi hizo zikiongezwa ziishie hapo, ninaomba juhudi hizo pia ziongezwe katika kusambaza gesi asilia katika taasisi na kwa wananchi. Kwa

sasa taasisi zilizounganishwa ni chache, lakini na wananchi waliounganishwa; ninazungumzia hasa wananchi wale wa mahalia, yaani wa Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua huku Dar es salaam maeneo ya Masaki na Oyster Bay sawa wamepata lakini ni muhimu wananchi wa Mtwara wakayaona haya matunda kwa sababu mnakumbuka hii gesi huko nyuma ilituletea madhara. Kwa hiyo juhudi ziongezwe katika kusambaza gesi asilia kwa taasisi zilizopo Mtwara na Lindi lakini na wananchi, kama Wabunge wengine walivyosema; kuona namna hiyo ya kuharakisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo likifanyika na lile la kwanza likafanyika itakuwa imepelekea pia matokeo chanya. Ninaomba pia uhamasishaji ufanyike kwa namna yoyote ile kupitia Wizara, uhamasishaji ufanyike wa kuona namna ya kupata wawekezaji watakaotuwezesha kuwa na viwanda vile tulivyokuwa tunavitarajia. Tuliambiwa kutakuwa na viwanda vya mbolea, basi uhamasishaji huo uendelee kufanyika, viwanda vya mbolea na viwanda vingine vinavyotokana na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pwani ilivyo pale, pwani sasa ardhi inakwisha kwa ajili ya viwanda. Kwa hiyo ninaamini na uhamasishaji huu ukifanyika wawekezaji watakuja watajenga viwanda vinavyotokana na gesi asilia katika maeneo ya Mtwara na Lindi. Kwa sababu mnafahamu viwanda vya Korosho vimekufa. Hata hivyo nimpongeze pia Mheshimiwa Bashe kwa juhudi kubwa anayoifanya sasa ya kufufua na hasa kutuletea zile kongani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii malighafi ya gesi tunayo Mungu ametupa na wakati ndio sasa. Inawezekana huko mbele kutokana na teknolojia tukawa tunataka vitu vingine sasa vya kidijitali zaidi, inawezekana gesi ikapitwa na wakati. Hatutaki kufikia huko. Ninatamani sana kizazi hiki tulichopo humu ndani tukaona matokeo ya gesi ile asilia inayopatikana Mtwara na hasa katika kuitumia hiyo malighafi kama ambavyo tumekuwa tukiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninaomba nishauri kwa Wizara ya Fedha; pamoja na mambo mengi yote ambayo kama nchi tunajua kwamba Mheshimiwa Mwigulu amekuwa akifanya vizuri, lakini ninamwomba sana, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa; zipo fedha kwenye maeneo mawili; ya kwanza ni fedha ya Mfuko wa Maji, tunajua inakwenda kwake, lakini ninaomba itoke kwa wakati ili na sisi watu wa Mtwara tunufaike nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hasa kilio changu kwenye maeneo mawili, ule Mradi wa Makonde ambao umetengewa shilingi bilioni 84.7 umekuwa ukisuasua. Nina uhakika hizi fedha za Mfuko wa Maji zikienda kwake zikaenda kwenye Mradi wa Makonde ina maana ile changamoto, ule mradi utatekelezwa kwa wakati; lakini hata ule Mradi wa Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, nivumilie dakika moja. Fedha za *export levy* zinapokwenda Mfuko Mkuu tafadhari sana tunaomba zirudi ili zikaendeleze zao la korosho. Kwa sababu tunajua wao wanatupa hivyo viuatilifu, lakini mambo mengine kama vile utafiti, mbegu bora na mambo mengine hata yale maghala zitatusaidia sana kuhakikisha zao la korosho na dhahabu hiyo ya korosho itakuwa inatuletea fedha za kigeni kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba niunge hoja mkono na niwapongeze sana Mawaziri kwa kazi nzuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo. Nilimwita Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, ajiandae.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii kuu ya Serikali. Awali ya yote nipende kumshukuru sana Mungu wa mbingu na nchi, muweza wa yote ambaye ametukirimia na kutufanikisha kuwepo katika Bunge lako

hili Tukufu. Pongezi zangu za pili ziende kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana ambayo anawafanyia Watanzania. Hakika amefanya kazi hii na kuzidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri hawa wamefanya kazi nzuri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, pamoja na msaidizi wake Hamad Hassan Chande na Mjumbe wa Kamati Kuu, Waziri wa Mipango Profesa Kitila Mkubo pamoja na Naibu wake Stanslaus Nyongo na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa; niwapongeze sana kwa kazi nzuri za kusimamia Wizara zao vizuri sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matunda haya tunayoyaona ni juhudi za Mheshimiwa Rais kwa kumshauri vyema, lakini pia kwa kusimamia Wizara zao vizuri; na ndiyo maana Taifa la Tanzania katika Afrika Mashariki na Kati ni Taifa ambalo kwa sasa ni la kuigwa na ni la mfano. Ndiyo maana hata jana tumeshuhudia Mheshimiwa Rais akifungua daraja katika historia ya nchi hii lenye kilometa tatu; na daraja hili halipo mahali popote katika nchi hizi za Afrika Mashariki na Kati isipokuwa hapa Tanzania. Hongera sana kwa Waheshimiwa Mawaziri, hongera sana kwa watendaji wote wa Serikali, hongereni sana Watanzania na hongera sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha bajeti za Serikali hata hii miradi ikaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti yangu ya mwisho kuchangia katika Bunge hili. Nianze kuwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge hapa tumeshirikiana vizuri sana na wamenishauri vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ukiwa kama Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo umekuwa Mwenyekiti wetu mzuri sana. Mheshimiwa Spika, amekuwa Mheshimiwa Spika wa viwango na amekuwa Mheshimiwa ambaye kwa kweli sisi Watanzania tunajivunia; pamoja na Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge,

watendaji wote wa hapa Bungeni na wafanyakazi wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niipongeze Serikali kwa yote ambayo imefanya katika sekta nyingi kule jimboni kwangu. Wananchi wangu wa Jimbo la Busokelo kwa takribani miaka mitano wameshuhudia miujiza na maajabu ambayo yamefanywa ndani ya Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi. Hapo awali katika sekta ya afya tulikuwa na kituo kimoja tu cha afya. Hivi ninavyozungumza tuna vituo vipya vya afya vitano na vingine vitatu vinaendelea kujengwa. Zaidi ya yote tulikuwa na zahanati zisizozidi tano hivi ninavyozungumza katika kipindi cha miaka hii minne takribani mitano tuna zahanati 14 mpya na zote hizi zimetekelezeka chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ametujengea hospitali ya wilaya nzuri sana ambayo ina vitendea kazi vyote na huduma za upasuaji zinafanyika pale katika Halmashauri ya Busokelo. Zaidi ya yote ametufanyia kazi ya kuwa na jengo zuri bora la kisasa. Ninasema lile jengo la halmashauri linaweza likawa ndilo jengo la kwanza kwa hapa Tanzania maana lina vyumba zaidi ya 205.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kazi kubwa na nzuri sana ambayo Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ametufanyia sisi Wanabusokelo; na sisi tunasema ifikapo Oktoba ya mwaka huu panapo majaliwa tunatiki kwa mama, tunatiki kwa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, hivi ninavyosema tuna shule mpya sita. Katika hizo shule sita, shule mbili ni za vipaji maalum, kwa maana kuna shule ya wasichana maalum na wavulana maalum, kwa maana ya *Busokelo Boys* na *Busokelo Girls.* Hizi ndizo shule pekee zinazofanya vizuri sana katika Halmashauri ya Busokelo na Wilaya ya Rungwe kwa ujumla na Mkoa wa Mbeya; zimefanyika kipindi cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mikakati yetu sasa tunataka tuwe *top ten* kitaifa. Kwa hiyo shule hizi ni kielelezo tosha kwamba elimu katika Jimbo la Busokelo imepaa sana na inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la barabara; tumekuwa na barabara ambayo tangu enzi na enzi ilikuwa haina lami. Hivi ninavyosema tayari Mkandarasi yupo *site*. Barabara hii ya Katumba – Suma – Mwakaleli – Mbambo mpaka Tukuyu yenye kilometa zaidi ya 83; na tunamshukuru Sana Mheshimiwa Rais, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alikuja kule akiwa pamoja na Waziri wa Ujenzi wakati huo, waliona ile barabara; na hatimaye hivi ninavyosema anashuhudia. Wamenituma wananchi wangu wa Busokelo wanasema ya kwamba tunawashukuru sana tena sana. Barabara hii ni mkombozi mkubwa sana wa wananchi kule kwa sababu wanalima, wanafuga. Pia kuna viwanda vya gesi ya asilia kwa maana ya *carbon dioxide gas*, vyote vimefanyika katika kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Mbunge anachochangia barabara anayoisema ni barabara ambayo mimi nimesoma shule ya kidato cha tano na sita kwenye jimbo lake, lakini barabara hii inaenda kuunganisha hadi Makete. Kwa jitihada hizi ambazo Mbunge wa Busekelo amefanya, ninaona kabisa Wanabusekelo wakienda kumchangua tena kwa mwaka 2025. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fredy, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, nimeipokea kwa mikono miwili, nami nimwombee kwa wananchi wa Makete ile barabara ile ya kilometa tisa ambayo alikuwa anazunguka zaidi ya kilometa 200 na kwa juhudi za mimi na yeye na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI nayo inafunguliwa. Kwa hiyo, wananchi wa Makete

wamwone kwa jicho la karibu ili ifikapo Oktoba apate nafasi tena ya kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumze pia suala zima la hizi barabara za mijini, kwa mfano pale Kandete Mjini kulikuwa hakuna lami, hivi sasa kuna lami na mataa yanawaka. Sisi kule tunasema ndiyo Dar es Salaam ya Busekelo kwa pale Kandete Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Lwangwa Mji ambapo ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri kulikuwa hamna lami, hivi sasa kuna lami na mataa yanawaka usiku na mchana, sisi ile tunasema ndiyo Dar es Salaam ya Busekelo. Sasa tuseme nini zaidi ya kumwombea Mheshimiwa Rais kusema mitano tena inamhusu na tumwombee afya njema ili ifikapo Oktoba sisi Wanabusekelo tutatiki kwa CCM na viongozi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya maji, kulikuwa kuna changamoto kubwa sana katika suala zima la maji Kandete Mjini, Lwangwa Mjini na maeneo mengine. Hivi sasa ninavyosema ambayo ndiyo Dar es Salaam ya Busekelo maji yanatoka masaa 24, imefanyika kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukienda Lwangwa hivyo hivyo na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna vijiji 56 havina umeme lakini sasa vijiji vyote 56 vina umeme, tunazungumza habari za vitongoji sasa. Kwa hiyo, ni habari njema kwa Wanabusekelo wote kwamba Mheshimiwa Waziri wa nishati ametuthibitishia ndani ya wiki mbili vitongoji 15 ambavyo vilikuwa vimebaki vitakwenda kupelekewa nguzo na vitakuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo za kilimo, sisi kule wananchi wetu ni wakulima na ni wafugaji na wote tunashuhudia Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri wa Fedha kutoa fedha kwenye sekta ya kilimo. Nilikuwa Mbunge katika Bunge lililopita, bajeti ya kilimo ilikuwa siyo zaidi ya bilioni 200. Hivi sasa tunazungumza zaidi ya

trilioni, matrilioni kwenye kilimo. Kwa kweli ni mabadiliko makubwa na ni mapinduzi katika sekta ya kilimo kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mbeya tulikuwa tuna changamoto ya *Airport*, Uwanja wa Kimataifa wa Songwe, hivi sasa wenzetu majirani ndege za Malawi zinatua pale, Zambia na Kongo zinatua pale. Kwa hiyo, hii itakuwa ni lango muhimu la Nyanda za Juu Kusini. Kiwanja hiki kitakuwa ndio mkombozi wa mikoa lakini pia wa nchi hizi ambazo nimezitamka. Haya yote yameshafanyika chini ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengi ya kusema, lakini natindikiwa kwa sababu furaha ikizidi unaweza ukaharibu, zaidi tu ya kusema tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, kazi yenu imeonekana. Mheshimiwa Profesa Kitila, yeye ni mwalimu wangu; na Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba, yeye ni mwalimu wangu na siku zote wamekuwa wakinifundisha namna ya kuweka mambo sawa Jimboni. Leo ninashuhudia kwamba na ninyi niwaombee kwa Mwenyezi Mungu *insha Allah* ifikapo mwezi Novemba waweze kurudi tena katika eneo hili la viwanja vya Bunge na wawe Wabunge tena pamoja na wasaidizi wao wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa muda wenu wote ambao tumekuwa hapa Bungeni kwa kushirikiana kwa pamoja na niombe kwa Mwenyezi Mungu aturudishe tena ikimpendeza na impendeze iwe hivyo ifikapo Oktoba mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete kwa mchango wako huo.

Nilimwita Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Tamima Haji Abass, ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mungu muumba wa mbingu na nchi kwa kupata nafasi hii tena niweze kuzungumza leo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa tarehe 20 Juni, bado siku saba twende tukawe raia wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichoko mezani ni Bajeti Kuu yenye trilioni 56.49. Nizungumze bila mashaka, kwanza nimwombee sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania azidi kuwa na imani na nchi yake ameiweza na kila kitu kinaonekana. Hata jana mimi nilikuwa Mwanza tumeshuhudia ufunguzi wa daraja. Kwa hiyo, hakuna shaka, hakuna tatizo kabisa na Watanzania wanamwelewa sana kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, nikushukuru wewe tumekuwa na wewe miaka mitano hapa ndani ya Bunge, ukweli mimi siyo mnafiki wala sipendi maneno ya uchawachawa Mungu akubariki sana tumekuwa nawe umetusimamia vizuri sana kwa nafasi yako. Nikuombee tu kwa wananchi wako wakuhukumu kwa haki wasije wakakufanyia *maneuver* ambayo hayaeleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimshukuru Waziri wa Fedha, kwenye bajeti yake ninakumbuka kuna maneno mengi nilishauri ya kimataifa na kitaifa, lakini tukiwa tunazungumzia leo trilioni 56 ninajua zote hizi zitapitia mkononi mwake na ninamwombea hata awamu ijayo aendelee kuwa Waziri wa Fedha kwa sababu hana baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu mimi kwenye Jimbo langu ninazo kilometa 102 ambazo ziko kwenye michakato mpaka sasa hivi na ninajua kutokana na hii bajeti tunayoizunguzia hapa zinaenda kutekelezwa. Kwa hiyo, anikumbuke anapofika Mbogwe mitandao isigome itiki moja kwa moja kama tunavyoenda kutiki Oktoba ili Wananchi wa Mbogwe waweze kupita kwenye barabara za lami ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimeiomba hapa ndani na ikakubali zikatekelezwe sasa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaporudi tena huku kwa sababu nina imani kuliko mtu yeyote yule kama maandiko yanavyosema imani ni kuwa na uhakika na mambo yale uyatarajiayo. Kwa hiyo, barabara hizi zikimalizwa nitakuwa na raha lakini pia na wenzangu niliowaacha huko Mbogwe watakuwa na amani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kipaumbele changu hapa tunayo maboma ambayo yamejengwa na wananchi; tuna maboma ya madarasa na maboma ya zahanati ni mpango wa Mwaka 2020 - 2025 kwenye Ilani yetu tuliahidi tukiwa tunatafuta kura kwamba hivi vitu tunaenda kuvikamilisha. Kwa hiyo, niiombe Serikali pale tutakapoanza tu makusanyo ya kodi hizi utekelezaji uangalie kwenye mambo hayo mawili miundombinu ya barabara, maboma pamoja na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, uniruhusu niwashukuru Wabunge wenzangu ambao nimekuwa nanyi ndani ya Bunge hili miaka mitano, hakika tumezoeana nina imani kila mmoja atam-*miss* sana mwenzake. Kwa sababu miaka mitano ni safari ndefu kweli, tumeishi kama nyumba moja familia moja na mimi niwaombe tu Wabunge wenzangu huko mwendako Majimboni Mungu awabariki sana na wakafanye kazi kwa kujiamini kwa sababu kazi kwa kweli imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo kuwa miaka mitano hii imekuwa na changamoto kwetu. Kwanza, kupotelewa na Rais wa Awamu ya Tano, hilo janga lilikuwa kubwa sana na kwa vile sasa hatujaanguka hapo, sina hakika kama tena jaribu lingine linaweza likatokea likatuangusha. Lazima twende kwa pamoja lakini vilevile tuendelee kuipa *support* Serikali yetu, hii ni nchi yetu sote si nchi ya mtu mmoja. Hata ikitokea bahati mbaya wengine wasirudi lakini kwa kuwa tumekuwa wazoefu wa kuifanya hii kazi ya uwakilishi tusisite kutoa ushirikiano kwa Serikali, kwa sababu maendeleo yanaanzia na Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli huko kwenye halmashauri zetu unakuta kuna halmashauri zingine zinakuwa na sheria ngumu sana, lakini kumbe ni uelewa tu unakuta. Kuna sheria huwa

zinapitishwa pasipo Madiwani wengine kujua kwamba wanachokitengeneza ni kitu gani. Matokeo yake halmashauri ile inakuwa na mambo magumu na inafanya watu kuichukia Serikali, kumbe ni kitu ambacho kimetengenezwa halmashauri tu na watu wachache ambao wana maslahi pengine binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zinapopita sheria hizo *(by law)* zinaenda kuwa kero Serikali kwa ujumla inataka kuchukiwa lakini kumbe Serikali tuliyonayo ni nzuri sana kwa sababu nimeiishi kwa miaka mitano. Nina uhakika sasa Serikali nzuri na Chama Cha Mapinduzi ni kizuri hakuna matatizo kabisa. Kwa hiyo, niwaombe watu wema wote wale walio na ndoto ya siasa na kule maendeleo na mabadiliko kwenye Taifa hili ni vyema waamini tu kwamba Chama Cha Mapinduzi kwanza kina viongozi makini sana ambao wanapenda haki, wana misimamo wanategemea nchi ipige hatua na ndiyo maana hata mimi mwenyewe niko kwenye chama hiki tunaendelea kulisongesha kuhakikisha kwamba tunapambana kutoka kwenye umaskini tulio nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninaomba uniruhusu nizungumze na wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe, wananchi wa Mbogwe mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, niombe kabisa kama vile walivyonizaa walivyonilea kati ya vitu ambavyo sitavifanya ni kuwa na kundi. Nitaendelea kuwa na misimamo yangu kwa sababu ninamwamini Mungu yaani haipo sababu hata ya kutengeneza safu. Kwa hiyo, wanichagulie Madiwani ambao watakuwa wanawafaa wao kwenye kata zao, kwenye mitaa yao, kwamba kwa vile wanaishi nao hao Madiwani wanawajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nimeshasikia maneno maneno kwamba mara huyu hatakiwi na Mbunge, mara huyu ndiyo anatakiwa na Mbunge, mimi sina mtu na sina mambo hayo. Kwa hiyo, wachaguane kwa kufahamiana. Ushauri wangu tu, wanipe Madiwani waaminifu na wakimwona mtu siyo mwaminifu haipo sababu ya kumwingiza kwenye siasa za nchi ya Tanzania, kwa sababu ukweli ni kwamba tumechelewa sana kwenye nchi yetu na sasa hivi ni wakati muafaka na Mungu

tunamwomba sana, hata watumishi wa Mungu tunawaomba watusaidie sana tupate viongozi waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa sababu ukifikiria Mbogwe mwanzoni ilikuwa haikusanyi kwanza mapato, ni kwa nini tulikuwa hatukusanyi? Tulikuwa tunakusanya mwisho milioni 700, nimeingia mimi bilioni 3.2 mpaka sasa hivi tumekusanya. Kwa hiyo, utagundua kwamba kulikuwa na mchwa au tulikuwa Madiwani wengine wabaya. Kwa hiyo, wakawahukumu kwa haki kwa kuwauliza kwanza kwa nini huko nyuma pesa zilikuwa hazionekani na miradi ilikuwa haiendi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawape majibu ili wawachague kwa haki na mimi sitaki nimtaje mtu hapa ila tu niiache hivyo. Kwa vile watu wa Mbogwe ni waelewa sana watakuwa wamenielewa kwamba ninamaanisha nini, wanipatie Madiwani wazuri ili kusudi Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania izidi kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninataka nikishauri hapa, katika Serikali yetu ya Tanzania kwa maana ya halmashauri zetu, tunao Wenyeviti wa Halmashauri kila Wilaya na Mwenyekiti wa Halmashauri anaenda mara mbili kwenye Halmashauri. Ni kwa nini wakati mwingine zinatokea hati chafu? Ni kwa nini halmashauri zingine zinatokea hati safi? Huyu Mwenyekiti kwa nini anaenda mara mbili kwa wiki anafanya nini? Kwa nini asitoe ripoti mapema kwenye Serikali pale kabla haijatokea hati chafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mwenyekiti kazi yake ni kwenda mara mbili kuikagua Halmashauri ili yeye akabaini na kutoa ripoti kwenye Serikali kwamba hiki kitu kinaenda hivi na hivi, kwa nini akae kimya tu huyu Mwenyekiti? Mpaka mwishowe tunakuja kupata ripoti mbaya za CAG. Kwa hiyo, hili Serikali iliangalie sana kwa ujumla kwa sababu ukiangalia hasara nyingi zinaanzia halmashauri,

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu inatuma pesa zinaenda kupokelewa halmashauri, miradi inayojengwa ya mabilioni ni kodi

za wananchi wanazolipa kidogo kidogo, lakini ni kwa nini inakuja kutokea hasara halafu watu hao wasichukuliwe hatua? Halafu ni kwa nini tuendelee kupanga bajeti kila wakati? Wakati mwingine tunaletewa shoti na watu ambao wanaeleweka. Kwa hiyo, ushauri wangu Serikali ijaribu kuchukua hatua mapema sana kwa hawa Wenyeviti wa Halmashauri pale hasara inapotokea kwenye halmashauri yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana kama vile wanavyowajibishwa kwenye nchi zingine, anakamatwa anawekwa kwa kesi ya uhujumu uchumi pamoja na wale alioshirikiana nao. Kwa sababu sisi Wabunge mara nyingi tunakaa tu huku Dodoma, Serikali inazidi kutoa miradi na tunaomba barabara sijui na nini, lakini pesa pale zinapofika hapo ni kwa nini zinapotea na Mwenyekiti yupo hapohapo? Halafu tuanze sasa kuilaumu Serikali au aanze kulaumiwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, lazima Serikali hili suala iliangalie sana. Kwa mamlaka haya ya kisiasa Mwenyekiti anapokuwa Halmashauri ifahamike shughuli zake ni nini na nini anapaswa kufanya nini ili inapotokea shoti wawajibishwe mapema haraka iwezekanavyo, tusiendelee kula hasara kwenye Taifa letu ili maisha yaende vizuri kuhakikisha kwamba tunapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuwashukuru Mawaziri wangu ambao nimekuwa nanyi miaka mitano, hakika miaka mitano hii ilikuwa safari ndefu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Chande, Naibu Waziri wa Fedha; nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mkumbo, ameendelea kunipa ushirikiano hapa; lakini pia *brother* Mheshimiwa Nyongo ameendelea kunipa *support* kwenye Wizara yake. Kila nilipokuwa ninakwenda na shida walikuwa wananisikiliza vizuri. Pia nisimsahau Mheshimiwa Ridhiwani, mtu wangu wa nguvu sana Waziri ambaye nilikuwa kila nikienda kwenye Ofisi yake ananipa ushirikiano na ninaweza kutimiza majukumu ya wananchi wangu. Hakika mimi sikuwa chawa, nilikuwa mwakilishi, nimefanya kazi hii kwa umakini mkubwa kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaka kabisa kuwa chawa wa mtu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale palipokuwa na ubaya nilikuwa ninasema hapa kuna ubaya, pale palipokuwa vizuri, ninasema vizuri na nitaendelea kuwa hivyohivyo. Kwa hiyo, Mawaziri ninawaombea sana Mungu awabariki sana na Mheshimiwa Rais awakumbuke kwenye Serikali yake ijayo ili tuje tuzidi kupiga hatua kuhakikisha kwamba tunasonga mbele kuisukuma nchi yetu ili tuweze kutoka kwenye wimbi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa …

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umeisha.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba ninakushukuru, lakini pia Waziri wa Fedha, nchi yetu tuko kwenye biashara za umoja kwenye hizi nchi *East African Community* Benki zetu bado riba ziko juu sana atusaidie…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga, usichangie tena malizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri afanye juu chini inavyowezekana ili kusudi tuweze kufanya ushindani vizuri, riba zishuke, tufanye biashara wengine, wengine haipo sababu ya kuja huku kwenye siasa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Tamima Haji Abass na Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu

kutupa zawadi hii ya uhai na pamoja na kupata nafasi hii ya kusimama hapa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukurani kwanza kwa Serikali, Serikali imefanya vizuri sana na kwa mimi kama ni Mbunge wa kutoka Zanzibar basi ninaishukuru sana Serikali. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajaribu kutaja sekta moja ambayo hii kwa kule kwetu itakuwa imekusanya vitu vingi sana ni sekta ya fedha za nje. Katika sekta hii ya fedha za nje, ninakushukuru sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Madelu hapa pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Hassan Chande wamefanya jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2021 tulianza na mkopo ule wa *RCF* (*Rapid Credit Facility)* ilifanya mambo makubwa sana kule Zanzibar, lakini tukaja na *ECF* tumefanya mambo makubwa sana kule Zanzibar, lakini kuna *Boosting Primary Education* tumefanya mambo makubwa sana. Isitoshe tokea kimeanza kipindi hicho tukitazama katika *GBS* (*General Budget Support)* hakuna mwaka ambao imesita na imekwenda kwa wakati na hiyo imefanyika kwa wakati na imeenda katika kiwango kamili. Kwa hiyo, Mheshimiwa ninakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Madelu na uongozi wote katika kufanikisha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine niipongeze *TRA, TRA* imekusanya mapato mazuri kama *trend* inavyoonesha kwamba ilikuwa ikiongezeka hata kuvunja *record* ya *quarter* kwamba ziko *quarter* ambazo zimekusanya vizuri sana katika *TRA*. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali, lakini pia na ndugu yangu Yusuph Juma yuko pale amekusanya na amefanya kazi nzuri sana, ndugu yangu Mwenda. Kwa hiyo, tunawapongeza sana *TRA* kwa makusanyo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe shukurani kwa wale watu ambao sasa hivi wananisikiliza ndiyo walionileta hapa, shukurani

zangu kwa wananchi wa Jang'ombe (Wapigakura wenzangu wa Jang'ombe) kwa kuniamini kwa kunileta hapa katika Bunge hili nafanya mambo ambao yanaifanya nchi yetu isonge mbele, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia, kwa kauli yao ambayo sasa wanasema mzungu wa nne tunaurejesha palepale. Kwa maana ya hiyo huu mzungu wa nne watakuja kuukuta tena katika meza hii kwenye hii mbao utakuwepo kwa mujibu wa maoni ya watu wa Jang'ombe ndiyo yako hivyo. Ninajua inawezekana ikawa wapo wanaopita kunusanusa, lakini tahadhari ninatoa tu kwamba usinusenuse kila kitu unaweza ukaja ukanusa sumu. Sasa ninawashukuru sana watu wangu wa Jang'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila wamenipa salamu, watu wa Jang'ombe wamenipa salamu hii hapa ambayo nimeiandika na hata ukipata kwenye Mitandao yote ya Jang'ombe utaikuta hii salamu wanasema: "Oktoba Tunatiki", ila wameniambia nifafanue. Kufafanua kwamba Oktoba Tunatiki, kuna Msemo wa Kiarabu unasema: *"Khalif tuarraf",* wewe ukitaka ujulikane upate umaarufu nenda kinyume, *khalif tuarraf*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna watu wana *khaalif* hiki kitu ili wapate umaarufu, natoa kisa kimoja, kuna mtu mmoja aliona mwezi alipoona ule mwezi magharibi ndipo unapoandama akasema mwezi ule umeandama, kwa hiyo yule mtu alipewa sifa na watu wote wakaenda kushangilia pale, sasa pembeni kuna mtu anaitwa Hababel na yeye akaona kwa nini huyu anapewa sifa, akaona na yeye aseme kaona mwezi, mwezi unaandama mmoja tu, akasema na yeye kaona mwezi, lakini kaonesha upande wa kaskazini, anaambiwa Hababel mwezi unakuwa mmoja tu huku kwa nini unatuonesha mwezi, anasema huu mwezi kumbe Hababel alikuwa anataka ule umaarufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaarufu huu unapelekea kumbe kuna watu wengine inawezekana wakawa hawaoni vizuri, kuna watu wengine wanakuwa wana tongotongo kwenye kope hizi, sasa anapogeukia yeye huwa anaona mwezi, mwezi ni mmoja tu

Oktoba, tarehe 25 Oktoba ndiyo mwezi. Sasa kama kuna Hababel ana mwezi unaoandama kaskazini yeye huyo ni mwingine, au hawa waliotaja mwezi kwamba utakuwepo mwezi mwingine, naona labda tongotongo zao, kwa hiyo wananchi wawaone hawa watu ambao wana tongotongo hakuna mwezi mwingine, mwezi ni Oktoba na Oktoba tunatiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri kwa Serikali. Jana Balozi Mulamula hapa jirani yangu alizungumzia athari ya fedha za nje kutokana na uhusiano ambao tunao wa kimataifa. Sasa alisema kwamba zimeleta athari kwamba fedha hazikuingia, lakini tukakosa tukapata upungufu wa ajira watu 1,200 kutokana na fedha ya *USAID*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu au niishauri ikajaribu kufanya utafiti, kuna baadhi ya fedha tunaweza tukaziona kwamba *multilateral,* lakini kumbe zikawa ni *bilateral.* Kwa maana gani? Tuna uhusiano na nchi fulani lakini zile fedha zipo katika mifuko mikubwa ya dunia, lakini ule mfuko wenyewe ukawa unachangiwa na nchi moja au ukawa unachangiwa na nchi mbili tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo litakalotokea katika ile nchi au kubadilika kwa sera ya ile nchi, au kubadilika kwa uongozi katika ile nchi unaweza ukaja ukatuletea shoti kama hii ambayo tuliyokuja kuiona. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali ikajaribu kutizama vile vitu ambavyo tunaweza tukaviona ni *multilateral,* lakini kumbe ni *bilateral* kwa sababu mchangiaji ni mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ukaona kwamba ni *international organization, multinational organization,* lakini ikaja ikazusha hili tatizo. Kwa hiyo ili kuepuka tusiende huko kwenye kupata shoti za namna hiyo ninaishauri Serikali kufanya jambo hilo, huo ushauri wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, tuna ndugu zetu hawa wa *OSHA* ambao wanashughulikia usalama na afya katika maeneo ya kazi, hivi sasa hivi mara nyingi sisi Wabunge hupiga makofi sana tukisema tumeondosha kodi ya *OSHA*, lakini kumbe wakati mwingine tunaikosesha haki ya binadamu

kutopatikana. Kuwa na usalama na kuwa na afya katika maeneo ya kazi ni haki ya kibinadamu, kwa sababu pale anaweza mtu akafariki kutokana na mazingira yale ya kazi hapana usalama na wala hapana mazingira ya afya nzuri, pia panaweza pakatokezea jambo lingine likampa mtu ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaishauri Serikali tunasema kwamba Dkt. Kitila Mkumbo akitaja atakwambia *investment* imeongezeka katika nchi hii, ile *huge of investment* iliyoongezeka hivyo zile fedha zinazokwenda kule *OSHA* zinatosha kuja ku-*cover* haya mazingira? Au wanakuja wawekezaji wanawekeza sisi tunazuia kutoa kodi za *OSHA* tunasema kwamba tumepunguza halafu tunabakiwa na walemavu na vifo na mayatima au tunapata watu wenye magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kukagua katika hayo maeneo, hii kodi au hii tozo tuichukulie kama ni haki au niishauri Serikali, basi tuweke *percentage* ya *income tax* ambayo inakusanywa iende katika *OSHA* ili iende ikaondeshe haya matatizo kwa sababu hii ni sawasawa na haki ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninazungumzia suala la kukuza ujuzi lipo kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwan pia. Suala la kukuza ujuzi kwa soko la nje. Leo Tanzania tuna diplomasia nzuri na nchi nyingine na ile nchi inatamani itoe watu kwetu waende wakafanye kazi kule, lakini hatuna ujuzi wa kwenda kufanya kazi kule. Ninatoa mfano kesi moja, kesi ambayo aliizungumza Waziri wa Mambo ya Nje, tumepeleka watu, lakini watu waliofaa ni watatu katika watu mia na zaidi. Sasa hii tunaondosha fursa, tujaribu kuangalia, kukuza ujuzi kwa ajili ya soko la nje, kwa sababu tumejijenga vizuri kidiplomasia tuitumie hii fursa hata katika kufundisha Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo bidhaa moja adimu Kiswahili lakini pengine inawezekana uwezo au ujuzi wa kwenda kuifundisha nje haipo vizuri. Sasa tujaribu kuangalia katika sekta hizi ili tuweze kuingiza mapato kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni upotevu wa mazao na hili ninakusudia kwa Dkt. Kitila Mkumbo ni la kilimo hili. Tumewekeza matrilioni ya pesa kwa pamoja katika miaka michache. Tumetoka kwenye bilioni 200 tumekwenda mpaka kwenye trilioni, inafika wakati wa mavuno tunaweza tukapata majanga tunaita ya mvua na wavunaji inawezekana sasa wasipate mazao, kwa nini tusiwekeze watu waweze kuvuna hata kama kuna mvua, Serikali yetu inaweza kwa sababu tulishawekeza kwenye kilimo, tulishawahamasisha watu walime, lakini je, tunayo mipango endapo yanatokezea maafa, pamoja na maafa hayo lakini wakulima wetu waweze kulima wapate kile kitu, vinginevyo tukiweka mbadala wa kulipa ruzuku kwa majanga kama haya itakuwa siyo vizuri kuliko tukamwezesha huyu mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninazungumzia ajira kwenye michezo. Michezo inaajiri sana, turudi kule zamani, uwekezaji sasa umepungua katika taaluma ya michezo. Zamani ukimgusa kocha utaambiwa kasoma Ujerumani, kasoma Brazil, kasoma wapi, kwa hiyo hata timu zetu za Taifa zikiongozwa ingawaje sasa hivi zinaongozwa na watu wa hapa si wageni, lakini tujaribu kuangalia kwamba sisi timu zetu hizi kubwa kubwa tuna-*import* makocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, hatuwezi kupata makocha wa kwetu? Kwa hiyo, taaluma kwenye michezo imepungua. Tujaribu kufanya kwa makusudi watu wapate taaluma ya michezo ili tusi-*import* hawa makocha na watatusaidia kuzalisha vipaji vingine. Pamoja na yote niseme kitu kimoja ambacho ninaishauri Serikali Kuu, kwamba wajaribu kuangalia wataalam wa michezo. Wataalam wa michezo wakapokee ushauri wao kwenye biashara kuna Baraza la Biashara moja kwa moja linakutana mpaka na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku tunajua lipo Baraza la Michezo lakini lipo zaidi kama baraza lenyewe, sasa tunataka hawa wataalam wa michezo wapo wataalam wa michezo wamehusika mpaka kwenda kupata ule uwanja wa *Arena* wa Rwanda, baadhi ya washauri wametokea hapa hapa kwetu

Tanzania. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali, ijaribu kukaa na wataalam wa michezo wapate ushauri, hawa wataalam wana mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninasema kwamba ninaunga mkono mia kwa mia, ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally King. Nilimwita Mheshimiwa Tamima Haji Abass, atafuatiwa na Mheshimiwa Benardeta Mushashu, tutamalizia na Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi mchana huu wa leo kuchangia hotuba ya bajeti na hoja zilizoletwa hapa mbele ya Wizara ya Fedha pamoja na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila kitu aliyenijaalia uhai, afya, nguvu katika muda huu wote wa maisha yangu. Pia ninawashukuru wote wale walioniunga mkono na kunisaidia katika kuniongoza mpaka nikaingia ndani ya Bunge hili Tukufu, vilevile Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionipokea mwaka 2022, wakanifundisha, wakanielekeza mpaka muda huu ninawashukuru Wabunge wenzangu nyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninampongeza Dkt. Mwigulu Nchemba, ninampongeza kwa hotuba hii aliyoiwasilisha hapa ambayo inatuonesha kwamba nchi yetu itakwenda kuwa na mafanikio makubwa baada ya utekelezaji wa bajeti hii. Vilevile ninampongeza Profesa Kitila Mkumbo kwa kutuwekea mpango madhubuti ambao utakwenda kutekelezwa sambamba na bajeti hii katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia wasaidizi wenu Mheshimiwa Chande, ninampongeza pia Mheshimiwa Nyongo, wote hawa kwa umoja wao wameweza kushirikiana wakaweza kutuletea mpango na bajeti hii ambayo ni mkombozi wa wananchi, hakika itakwenda kuwakomboa wananchi wetu kwa kipindi chote cha miaka mitano ijayo, nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana vilevile Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwingi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi tunayoimalizia 2020 - 2025. Hakika wamezitendea haki sekta zao walizozisimamia na hata sasa tumeona Tanzania nzima imekuwa ikiwataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Tanzania Bara, Dkt Samia amekuwa akitajwa kila sehemu, ukienda Zanzibar Dkt. Hussein Ally Mwinyi amekuwa akitajwa kila sehemu. Hii yote ni kutokana na utekelezaji wa Ilani waliyoifanya na kusikiliza kwa sababu kila Mkoa ameonesha hapa viongozi wote waliosimama wa Waheshimiwa Wabunge wameeleza katika maeneo yao kazi zilizofanyika. Hakika kazi walizozifanya ni za kutukuka na *Insha Allah* Mwenyezi atawajaalia, atawalipa mema kwa kile ambacho wamekitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na shukrani zangu, ninatoka Mkoa wa Kaskazini Unguja nikiwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao kwa hakika wamefarijika na jitihada za Marais wetu hawa na viongozi wetu hawa waliomo ndani ya Serikali na zaidi viongozi hawa wametokana na Chama Cha Mapinduzi. Chama Cha Mapinduzi kimetuwekea misingi imara ya kuwapata viongozi wazuri ambao watatuletea maendeleo sisi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hapo nianze kwa kusema ndani ya Mkoa wa Kaskazini hususan wanawake wa Mkoa wa Kaskazini tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha viongozi hawa wanarudi madarakani ili waweze kuendeleza yale waliyoyapanga wananchi waweze kupata manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuja kutufungulia kituo chetu cha ujasiriamali pale Mkoa wa Kaskazini Unguja cha wanawake na alipokuja akatuasa mambo mengi na alitoa kauli pale akasema kwamba viongozi watapimwa kutokana na utendaji wa kazi

waliyoifanya. Akatushajihisha akatuambia kwamba katika kituo kile cha ujasiriamali ambacho kitakuwa kinafundisha ushoni, akatuahidi kutoa vyereheni vitano, lakini kwa uzalendo wake mama huyu alitupa vyerehani 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kuonesha kwamba anawiwa na changamoto za wananchi kukosa ajira, kwa sababu kituo kile kinapokea vijana wengi ambao wanakuja kujifunza pale, wakitoka kujifunza watakwenda katika maeneo yao kwenda kuyaendeleza na hatimaye watapata kipato. Sasa kwa hilo ninampongeza sana, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia vyerehani vile, tunamshukuru na tunamwahidi tutazifanyia kazi kwa kadri ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea vilevile kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika ziara zangu nilizokuwa ninatembelea nilikuwa nimepitia katika dawati la jinsia pale Mahonda, wakanieleza changamoto nyingi wanazopambana nazo, lakini mwisho wa siku wakasema wanashukuru sana kwa sababu kuna watoto ambao walikuwa wanapatikana na shida kidogo, basi walikuwa wanapeleka kituo cha polisi na nikaona bora nitembelee, nikatembelea kituo cha polisi na nikatembela Kituo cha Polisi cha Mkokotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mkokotoni kimejengwa upya, kilijengwa tangu miaka ya ukoloni lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akawapelekea pesa kikajengwa upya kituo kile kipo vizuri na makamanda wa pale waliniambia niwaletee shukrani zao kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hili ninaomba amwambie Mheshimiwa Rais kwamba zile pesa alizopeleka wakajengewa kituo kile cha polisi, basi wanamshukuru sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo ni kizuri, kituo kina miundombinu ya kisasa kwa sababu hapo mwanzo ilikuwa hata wale watoto wanaokinzana na sheria walikuwa wanawekwa pamoja na mahabusu watu wazima, lakini kwa sasa kituo kimejengwa, kina miundombinu mizuri hata mahabusu ya watoto ipo nimeiona ipo vizuri. Kwa hiyo ninamwomba sana Mheshimiwa

Waziri ampe salamu hizi Mheshimiwa Rais kwamba makamanda wa Kituo cha Polisi Mkokotoni wanamshukuru sana kwa lile alilowafanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea mbele, ninashukuru tena kwa Mheshimiwa Rais ametupatia majiko ya gesi kwa ajili ya wananchi wetu, kwa hiyo na kwa Mkoa wa Kaskazini ninashukuru wamepata, ametupa mashuka mama, tumekwenda kupeleka kwenye hospitali zetu, pia na hilo tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo Mkoa wa Kaskazini tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuzisaka kura tuhakikishe tunamrudisha tena mama huyu na pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi wapate kura za kishindo. Tunashukuru sana kwa kazi zote walizotufanyia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye hii bajeti ya Serikali pia naishukuru kwa sababu ukiiangalia hata vile vipaumbele vyake vilivyowekwa pale vinamlenga mwananchi wa kawaida moja kwa moja atanufaika. Vipaumbele hivi vitawasaidia wananchi kupata ajira, kwa sababu kuna kuwastawisha wananchi kwa miradi yote na mipango na ajira, kila kitu. Sasa haya yote wananchi wananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye sehemu ile ya ajira, watafaidika wananchi, tukiangalia bajeti iliyokwisha ya 2025/2026 tuliona kwamba ajira kwa mujibu wa Ilani yetu ya Uchaguzi kipindi kile walikuwa wamesema ajira 8,000 wananchi watapatiwa, lakini utekelezaji wa Ilani ile umevuka kwa sababu kuna ajira zimetoka 8,000 na nukta nane. Sasa kwa sababu hiyo tunashukuru sana Serikali, tunashukuru sana kwa kazi zote zilizofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo kila nikiendelea mimi nitakuwa ninashukuru tu, lakini yote ni kwa sababu kazi kubwa imefanyika ya kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu. Ninashukuru sana uongozi wa Chama changu Cha Mapinduzi kwa muda wote unijaalia nikaingia humu ndani ya Bunge hili Tukufu, ninawashukuru sana uongozi wa Kaskazini Unguja, wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, UWT kwa pamoja, mama yetu Mama

Mary Chatanda anatusimamia vyema, tunashukuru tunaendelea mpaka muda huu tunapokamilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Nimwite sasa Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Tarimba Gulam Abbas.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba; Naibu Waziri wa Fedha Hamad Hassan Chande; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo; na Naibu Waziri wake Stanslaus Nyongo; Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili; Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango; na Gavana wa Benki Kuu Ndugu Emmanuel Tutuba kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bajeti hii ni nzuri, inawagusa wananchi walio wengi, katika bajeti hii kuna hatua nyingi za kikodi ambazo zimewekwa ambazo sasa zinaenda kutusaidia kulinda viwanda vyetu vya ndani, pia inaenda kutusaidia kuweza kukusanya kodi zaidi, tunapokusanya kodi ndiyo tutaendelea kupata maendeleo na vilevile kuchochea uwekezaji. Tunasema hii bajeti ni nzuri, ni bajeti ya watu kwa sababu itatusaidia kutatua matatizo mengi ambayo yamo kwenye maeneo yetu na itatusaidia kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi hizi kwa Wizara hizi kwa kazi nzuri wanayofanya, Wizara hii wanahakikisha kwanza fedha zinapatikana, sidhani kwamba ni kazi ndogo kuweza kukusanya trilioni 56.49, kwa hiyo kazi imefanyika, vichwa hapo vimechemka wakaweza kuzipata na kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo inapata hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza vilevile kwa usimamizi mzuri wa sera za fedha. Hawa wamewezesha haya kufanikiwa kwa sababu ya ubunifu, uchapakazi, weledi na uadilifu wao. Pia, wamekuwa wasaidizi wazuri sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi, bado Taifa linawahitaji. Kwa hiyo, ninawaomba wananchi wa Jimbo la Iramba wamrudishe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa sababu bado tunamhitaji; ninawaomba wananchi wa Jimbo la Ubungo wamrudishe Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, bado Taifa linamhitaji; tunaomba wananchi wa Jimbo la Kojani waweze kumrudisha Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, aweze kuendelea kwa sababu Taifa bado linamhitaji; na tunaomba wananchi wa Maswa Mashariki wamrudishe Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo kwa kura nyingi kwa sababu Taifa bado linawahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefanya kazi nzuri, tunaomba warudi na ikiwezekana ikimpendeza Mheshimiwa Rais awapatie nafasi nyingine kama hizi kusudi waendelee kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inasimamiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo makubwa. Kwa kweli leo hii Tanzania ukienda kila kata, ukienda kila mkoa, ukienda kila wilaya kuna mradi wa maendeleo unaoendelea au kuna hela zimeingia. Hii ni kwa sababu ya kazi nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkoa wa Kagera kwenye afya tuna halmashauri nane na zote tumejengewa hospitali za halmashauri; vituo vya afya 24; zahanati 40; na kwenye *Bukoba Regional Referral Hospital* tumejengewa jengo zuri sana la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji kuna miradi mingi imetekelezwa Mkoa wa Kagera ukilinganisha na upatikanaji wa

maji wa 55% uliokuwepo 2015 leo hii tumefikia zaidi ya 70% huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia kuna Mfuko wa 10% ule wa Halmashauri ambao sasa unawasaidia wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuendeleza biashara zao ambapo nao biashara zao zikikua ndiyo wanaweza kulipa kodi. Hapa wameweza kukusanya shilingi bilioni 12.86. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kuipa *TARURA* na *TANROADS* fedha za kutosha na barabara nyingi vijijini na mijini zinajengwa. Tumejengewa madaraja nane, barabara za lami na za changarawe mpya zinajengwa na tunajengewa daraja moja kubwa la Kitengule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu katika kipindi cha miaka minne tumeshuhudia matokeo makubwa sana katika Mkoa wa Kagera ukilinganisha na tulianza na madarasa 1,606, leo hii tuna madarasa 7,610 katika kipindi tu cha miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejengewa pia, shule mpya zikakamilika 12 za msingi, 19 za sekondari. Tumejengewa shule nzuri ya kisasa ya wasichana; itawalinda watoto wetu wa kike, watasomea pale, watakuwa Watanzania bora na watatimiza ndoto zao. Shule hiyo inaitwa *Kagera River Girls Secondary School* na sasa sisi akina *ishomire* tunajengewa chuo kikuu. Tunasema Mama Samia ahsante sana, hatuna cha kumlipa, tunangoja tukamlipe mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa pamoja na hayo mambo makubwa tuliyoyapata, tunaomba ikiwezekana waendelee kuangalia uwezekano wa kujenga masoko ya mipakani. Tuna uhakika wakijenga masoko mipakani na kule Mkoa wa Kagera tuna mipaka mingi, hii itachechemua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anapohangaika kutafuta fedha, hiki ni chanzo kimojawapo kizuri

ambacho kinaweza kikaleta mapato. Wanategemea pato likue kwa asilimia sita kwenye mwaka ujao lakini kwa kufanya vitu kama hivi tunaweza tukakuta tunaruka mpaka tunafikia asilimia nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo bado wilaya sita kati ya nane ambazo hazijaingia kwenye Gridi ya Taifa kwa maana ya Kyerwa, Karagwe, Misenyi, Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini na Muleba. Tunaomba nazo ziingizwe kwenye Gridi ya Taifa kwa sababu mnajua kwamba umeme ni uchumi na umeme unaweza kutusaidia kutoka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa sana kwenye kilimo. Waheshimiwa, wote wanajua kwamba zao kubwa katika Mkoa wa Kagera ni kilimo cha kahawa. Watu wameteseka sana na bei ya kahawa ambayo ilikuwa chini ya shilingi 1,000, mwishowe wastani ukaja mpaka kwenye shilingi 1,100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, amekuja Kagera mara kadhaa, amekutana na wakulima, amekutana na vyama vya ushirika. Serikali imeondoa tozo mbalimbali na sasa hivi bei imepanda kutoka kwenye shilingi 1,100 imefikia shilingi 5,000 kwa kilo moja. Tunasema, sasa ahsante sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana Mama Samia. Tunangoja tu tumlipe kwenye sanduku la kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kuwa huu ni mkutano wa mwisho wa Bunge la Kumi na Mbili, ninaomba niwapongeze wote tulio hapa kwa kuhitimisha kazi nzuri ambayo tulitumwa kufanya. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema pamoja na uhai wa kuweza kuyafanya haya yote tuliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya yeye kama kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Bunge. Tunamwombea baraka tele ili wananchi wa Ruangwa wampe kura za kutosha na aweze kurudi hiyo Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri anazofanya. Tangu alipopewa nafasi hii kwa kweli ameitendea haki. Tunawaomba wananchi wa Jimbo la Bukombe wamrudishe Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko Bungeni kwa kura nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru Wenyeviti wote wa Bunge. Wamefanya kazi nzuri ya kuongoza shughuli zote za Bunge hili na tunawaombea wote wakarudishwe humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu. Tunawaomba Watu wa Ilala wakampigie kura nyingi. Tunamjua ni mzee wa *speed* na viwango, aweze kurudi humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Katibu wa Bunge, Tume pamoja na Wakurugenzi na watumishi wote, kwa kweli wametuwezesha tukaweza kuyapata haya mafanikio tuliyofanikiwa. Bila wao tusingeweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Spika wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson Mwansasu, Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Amekuwa kiongozi wa kuigwa, mwenye unyenyekevu, weledi wa kutosha, hekima na busara tele; ameliendesha Bunge hili kwa viwango vya kisasa na kwa ufanisi mkubwa. Tunaomba wananchi wa Jimbo Jipya la Uyole wamwone, wampe kura nyingi, ashinde na arudi Bungeni. *Your future is even brighter*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa Ilani ambazo zimeendelea kutekelezwa ambazo zimeleta maendeleo katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kagera walioniona, wakanichagua na wakanipa Ubunge nikafika hapa. Tumefanya kazi pamoja, kazi kubwa na nzuri. Ninawahakikishia... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako ulikuwa umeisha. Nilikuwa nakuacha umalizie.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia. Ninamalizia kwa kusema, ninawahakikishia kwamba bado nipo na nina nguvu za kuwatumikia. Niko njiani ninakuja twende kutafuta kura za Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwenyezi Mungu awabariki Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote humu ndani. Kila mtu aende akashinde kwenye jimbo lake, tukutane hapa Desemba. Kwa Mama Samia tunasema, mitano tena, yajayo yanafurahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, aweze kukamilisha shughuli ya leo.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa mwisho katika hotuba hii ambayo inakwenda kuhitimisha muhula wa miaka mitano wa uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, niweze kumpongeza sana Waziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Hongera sana kwake na Naibu wake, ndugu yangu Mheshimiwa Chande, ambaye sasa ni Mjumbe wa Kamati Kuu katika chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile jirani yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Nyongo. Hakika ukimjumlisha na Kamishna Mkuu wa *TRA,* Yusuph Juma Mwenda; hawa watu wamefanya kazi vizuri sana. Lazima niwapongeze na tuwapongeze, wameifanyia kazi Tanzania, wameipendezesha Tanzania, wameisaidia Tanzania uchumi wake kuweza kukua. Pia, hapa lazima nimpongeze

Mheshimiwa Rais kwa kuwaona wao ambao hakika wameweza kumsaidia na hakuna mtu ambaye anaweza akabisha kwamba Tanzania hii sasa imepiga hatua kubwa sana kiuchumi na inafahamika kimataifa, siyo kama tulivyoikuta mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiangalia maandiko yanaonesha katika nchi 42 za *Sub-Sahara Africa*, Tanzania kwa uchumi ni nchi ya saba. Ni hatua moja kubwa sana na hali hii inatuonesha kwa sababu kuna maandiko mengine yanasema, kwenye Afrika nzima sisi ni miongoni mwa nchi 10 na wengine wanasema ni nchi ya 11. Vyovyote vile itakavyokuwa, 10 na 11 haziko mbali. Hivyo, hongera sana. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Baraza lako lote la Mawaziri kwa sababu wameweza kuiheshimisha Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana juzi wakati nikiwa katika ziara zangu kule jimboni, wananchi wa Kinondoni wameonesha kuridhika sana na utendaji wa Serikali na utendaji wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wenyewe wanasema wanasubiri mwezi Oktoba ili Kinondoni iweze ku-*tick* na ninaamini Dar es Salaam na Tanzania nzima tunakwenda ku-*tick*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa katika kuchangia kwangu nizungumzie njia mbadala ya kuchangamsha uchumi kupitia Jiji au Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Dar es Salaam ni eneo ambalo ndilo lenye msukumo mkubwa wa shughuli za kiuchumi na biashara katika Tanzania yetu. Pia, hata mapato ya Taifa makubwa sana yanatokea Dar es Salaam ambapo Dar es Salaam peke yake tunachangia zaidi ya 17% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023, Dar es Salaam ilichangia takribani shilingi trilioni 32.1 kati ya shilingi trilioni 188.8 ya pato la Taifa. Kutokana na ukubwa huu wa uchumi wa Dar es Salaam na mchango wa Dar es Salaam, kuna haja ya kuiangalia zaidi Dar es Salaam na hasa katika maeneo ambayo yakifanyika

yanaweza yakachagiza zaidi uchumi wa Taifa kwa maana ya pato la Taifa na vilevile uchumi ambao utaweza kwenda kusaidia mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa zaidi nizungumzie suala la barabara kwa sababu barabara ni moja kati ya vitu muhimu sana vinavyoweza kusaidia uchumi ukakua haraka. Usafiri na usafirishaji ni *ingredient,* ni vitu muhimu sana katika masuala mazima ya uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam tuna kilometa zaidi ya 2,000 *(to be precise* ni kilometa 2,206). *TARURA* hivi karibuni walifanya upembuzi wakaona ni barabara gani muhimu ambazo kama zitaweza kutengenezwa zinaweza zikasaidia sana kuibadilisha Dar es Salaam iendane na ukuaji wa uchumi, itengeneze matumaini kwa *investors* wanaokuja pale, kuuona mji kwamba una barabara ambazo hakika zinaweza zikasaidia usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilometa 756 ambazo tunaweza tukaziita barabara muhimu. Kati ya hizo, kilometa 44 ziko Kinondoni na tunafahamu vilevile kwamba kuna Mradi wa *DMDP II* ambao huu sasa unakwenda kujenga takribani 30% ya barabara zote hizo nilizozitaja ikiwa ni sawa na kilometa 225.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu zinaonesha itatuchukua si chini ya miaka sita kuweza kumaliza kuzitengeneza hizo barabara za kilometa 225. Sasa ukizichukua barabara za kilometa 756 ambayo ndiyo mahitaji yetu, ukiondoa 225 tunabakiwa na kilometa karibu 500 na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi kwa kutegemea bajeti ya Serikali ya kila mwaka itatuchukua miaka mingi sana na kwa hali hiyo haitawezekana kuchepusha uchumi wetu kwa haraka zaidi. Tunachohitaji ni maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia ametuonjesha ni kwa jinsi gani Tanzania inaweza ikapiga hatua za uchumi wa haraka kwa haya ambayo ameyafanya katika kipindi

cha miaka minne. Ninaamini Serikali inaweza ikaangalia njia mbadala ya kutafuta fedha. Ukiondoa huu Mradi wa *DMDP* hesabu zinaonesha kwamba, tunahitaji takribani shilingi trilioni 1.89 ili Barabara za Dar es Salaam ziweze kutengenezwa zote hizi kilometa 700 na ushehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali iangalie siyo lazima iwe kwa mwaka huu, lakini hata kwa mwaka ujao katika mipango yetu, tukaweka utaratibu wa kuangalia *alternative sourcing* ya fedha; siyo lazima tuitoe kwenye bajeti yetu. Kuna watu wengine ukiwashauri kwamba hata tukienda kukopa ni vizuri tu kwa sababu Dar es Salaam inahitaji ijengwe sasa hivi kwa mafanikio ya sasa hivi kwa Tanzania ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusisubiri tudundulize, (kudunduliza lugha yangu ya Tanga kidogo ngumu). Kile kidogo kidogo mpaka upate nyingi halafu uje ujenge hizo barabara zote, hiyo itatuchukua miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam lazima liwe Jiji la matumaini; Jiji ambalo wawekezaji watakapokuja waweze kuona kweli pale ndipo Dar es Salaam. Sasa hivi Dar es Salaam ikifika usiku maeneo machache sana utakuta kuna taa za barabarani; hapana haipendezi. Hivyo, hata huu mradi kama Serikali itaona ni vizuri kutafuta njia mbadala za kutafuta fedha, barabara za Dar es Salaam zikajaa taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda miji ya watu vilevile tunakuta hata *business names* yaani majina ya biashara yamewekewa taa. Kuna kitu wanaita *neo signs*. Tukienda Dubai, tukienda Nairobi, tukienda *South Africa* tunaona lakini kwetu Dar es Salaam ukiweka *business name* yako (jina lako la biashara) kwa kuweka taa au kwa maandishi makubwa kesho unatozwa kodi. Ningeshauri vitu vingine vidogo vidogo ambavyo vinakwamisha kutufanya Dar es Salaam tukue kwa haraka lakini tuupendezeshe mji wetu vilevile, tuko katika zama nyingine tuweze kufikiria na tuwe na mawazo mengine nje ya *box*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda zaidi nizungumzie Dar es Salaam na ushauri wangu ni kwamba, tuiangalie zaidi Dar es Salaam ili Dar es Salaam iweze kuchangia zaidi kwenye uchumi wa Taifa letu kwa manufaa ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja hii na ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Rais kwa yale aliyoyafanya katika Jimbo la Kinondoni ambayo nisingependa kuyarudia, ninataka nimwambie, wana Kinondoni tuko tumeridhika sana na kazi yake. Tunasubiri mwezi Oktoba twende tuka-*tick*. Hilo hatuna mashaka lakini tuwaombee Mwenyezi Mungu awajaalie Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili ambalo wamefanya kazi iliyotukuka ambayo hakika wametuleta katika mafanikio makubwa ya uchumi wa Taifa hili, basi Mungu awajalie waweze kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona Kinondoni mimi nipo ndugu yenu Tarimba Abbas, mwananchi; Mwananchi wa Tanzania, siyo Mwananchi Yanga maana yake wengine nikisema mwananchi wataingia wasiwasi. Nitakuwa pamoja na nyie Mwenyezi Mungu akijaalia katika kipindi kingine cha miaka mitano. *Bi idhnillah, Assalamu alaykum wa rahmatullahi taala wabarakatuh*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Tarimba kwa kukamilisha.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia tamati ya kikao chetu cha leo. Ndani ya Ukumbi wetu wa Bunge tulikuwa na wageni mbalimbali. Niwalete kwenu kuwatambulisha kabla hatujafunga.

Tunaanza kwanza na wageni wa Mheshimiwa Spika. Hawa ni wanachama 80 wa Jukwaa la Wazalendo Huru Tanzania kutoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Nao wamo katika ukumbi wetu, ninadhani wako upande wa, wako pale. *(Makofi)*

Wageni wetu hawa kesho watakuwa na kongamano kubwa kwenye Ukumbi wetu wa Jakaya Kikwete na kongamano litakuwa ni la amani, upendo, uzalendo na mshikamano kwa Taifa ambalo litaanza saa nne asubuhi mpaka saa 10 jioni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana kwenye kongamano la kesho. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni 44 wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni Kikundi cha Sauti ya Wanawake Jasiri kutoka Chalinze Mkoa wa Pwani. Karibuni sana na ninawashukuru kwa kututembelea. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, ambaye ni Ndugu Lightness Laizer. Huyu ni Mkurugenzi wa Fey *Logistics* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tuna wageni 18 ambao ni Watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Arusha pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Meru wakiongozwa na Ndugu Suleiman Msumi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katika kundi hilo kuna Mwalimu Zainab Mwakinya ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 39 na Walimu watano wa Shule ya Msingi Lucky Vincent iliyoko Kata ya Olasiti, Halmashauri ya Jiji la Arusha. Wanafunzi 39 mko pale na walimu wenu; karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni watatu kutoka Kata ya Ipagala Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yalikuwa majina ya wageni ambao tulikuwa nao. Pia, mnakumbushwa kwamba pamoja na kongamano hilo ambalo litaanza saa nne, tuna jambo letu asubuhi kuanzia Saa 12 la Bonanza na litaisha saa sita. Kwa hiyo, ninadhani tunaanza na Bonanza asubuhi halafu baadaye tunakwenda kwenye kongamano. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, niwashukuru sana kwa michango yenu kwa wale ambao wamepata nafasi siku ya leo kuchangia na wale ambao wameendelea kuchangia kwa kadri ambavyo tulikuwa tumejipanga.

Tunakwenda mwishoni mwishoni na Siku ya Jumatatu Waheshimiwa Mawaziri wa kila sekta watapata nafasi na wao ya kuchangia. Kwa hiyo, tuna mategemeo kwamba watajiandaa vizuri kabla mtoa hoja hajafuata. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha Kikao hiki cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 23 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*